

PFMRP



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



TOLEO MAALUM
KWA WANANCHI

RIPOTI ZA MDHIBITI NA
MKAGUZI MKUU WA HESABU
ZA SERIKALI (CAG) KWA
MWAKA 2015/2016



UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninatambulisha kitabu cha Toleo Maalum kwa Mwananchi kwa msomaji wangu. Toleo hili ni muhtasari wa ripoti za ukaguzi wa kila mwaka.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi wa Umma Duniani (INTOSAI) ambayo ofisi ninayoiongoza ni mwanachama zinahimiza umuhimu wa upashanaji habari mionganoni mwa jamii. Ibara ya 18 (2) inasema, “Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za mwananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii”.

Toleo hili ni la nne ambalo linawasilisha taarifa za ukaguzi wa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2016 na ukaguzi wa ufanisi zilizoishia tarehe 31 Machi 2017.

Toleo hili linatoa taarifa za matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha (i) Ripoti ya Serikali Kuu; (ii) Ripoti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; (iii) Ripoti ya Mashirika ya Umma; (iv) Ripoti ya Miradi ya Maendeleo; pamoja na Ripoti 9 za Ukaguzi wa Ufanisi ambazo zimejumuisha maeneo ya Maji, Afya, Elimu, Usafirishaji (Samani za Barabara na Vyombo vya Usafiri Katika Maji), Maeneo ya wazi, Mafuta na gesi, Ajali za moto katika majengo ya umma na ufuatilaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya CAG yaliyotokana na kaguzi za Ufanisi.

Ni imani yangu kuwa taarifa hizi zitakuwa chachu ya uwajibikaji wa makundi mbalimbali yenye dhamana ya kuhakikisha kwamba tija na ufanisi



vinakuwa sehemu ya kila mwenye dhamana ya kusimamia rasilimali za umma.

Ninapenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa washirika wa maendeleo kwa msaada wao ulioniwezesha kuandaa na kutoa toleo hili.

Vilevile, ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa kazi kubwa waliyofanya ili kuhakikisha toleo hili linapatikana kwa wakati.

Ninawahimiza wananchi wote kukisoma kitabu hiki kwani watafahamu kwa kina kazi zinazofanywa na ofisi yangu.



Prof. Mussa J. Assad

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Juni, 2017

DIBAJI

Kitabu hiki kimegawanyika katika sura tisa zinazowasilisha taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni 2016 pamoja na ukaguzi wa ufanisi kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2017.

Sura ya kwanza inatoa taarifa ya utangulizi wa kitabu, wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, madaraka yake, dira, dhima, misingi ya uadilifu pamoja na ufanuzi wa baadhi ya maneno yaliyotumika kwenye kitabu hiki.

Sura ya Pili inajumuisha maelezo ya jumla kuhusu ukaguzi, aina na tafsiri ya hati pamoja na idadi ya hati za ukaguzi zilizotolewa kwa ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2016.

Sura ya Tatu inajumuisha utekelezaji wa mapendekezo ya nyuma yaliyotolewa katika ripoti za ukaguzi wa hesabu za serikali.

Sura ya Nne inatoa taarifa za ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu ambapo ni mafungu 62 ambayo yanajumuisha Wizara na Taasisi za Serikali; Hesabu Jumuifu za Taifa 1; Mamlaka ya Mapato Tanzania 1; Sekretarieti za Mikoa 25; Wakala wa Serikali 33; Mifuko Maalum 13; Balozi za Tanzania 34; Bodi na Mamlaka za Maji 13; Taasisi nyinginezo 34 na Vyama vya Siasa 5.



Sura ya Tano inatoa taarifa za ukaguzi wa hesabu za Serikali za Mitaa ambayo inajumuisha ukaguzi wa taarifa za Halmashauri za Wilaya na Manispaa 171 zilizokaguliwa kwa mwaka 2015/16.

Sura ya Sita inatoa taarifa za ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma ambayo imeainisha masuala yanayoathiri mashirika na taasisi 112 zilizokaguliwa katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2016. Kaguzi hizo zinajumuisha taasisi za kifedha 14, mifuko ya mafao 6, mamlaka za umma 45, taasisi za elimu ya juu 19, Mamlaka za usisimamizi 14 na taasisi nyinginezo 14.

Sura ya Saba inatoa taarifa za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ambapo miradi mikubwa minne inayofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wahisani kupitia mfuko wa pamoja. Miradi hiyo ni Programu ya Maendeleo ya sekta ya Kilimo (ASDP) - 128, Mfuko wa Afya (HBF) - 163, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) - 68 na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) - 163. Aidha, ukaguzi umefanyika katika miradi mingine 112 inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa (UN) na wadau wengine wa maendeleo. Vilevile, sura hii inatoa taarifa ya ukaguzi wa Mfuko wa Barabara unaofadhiliwa na mapato ya ndani yatokanayo na tozo za mafuta.

Sura ya nane inatoa taarifa ya kaguzi tisa za ufanisi zilizofanyika kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2017.

Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi wa ufanisi ni pamoja na Usimamizi na Udhibiti wa Uchukuaaji wa Maji kutoka vyanzo vya Maji; Uendelezaji wa

Miundombinu ya Shule za Msingi, Usimamizi wa Samani za Barabara; Usimamizi wa Mikataba ilioingiwa kati ya Serikali na Hospitali binafsi; Wahitimu wanaoandaliwa kwenye Sekta ya Mafuta na Gesi nchini; Usimamizi wa Kaguzi za Vyombo katika Usafiri wa Maji; Uendelezaji wa Maeneo ya Wazi yaliyoainishwa Nchini; Usimamizi wa Usalama dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma na Ukaguzi wa Ufutiliaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilizofanyika na Kuwasilishwa Bungeni mwaka 2012 na 2013.

Sura ya tisa na ya mwisho inatoa taarifa za Kaguzi Maalum nne zilizofanyika katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2016.

Kati ya kaguzi nne zilizofanyika, mbili zilifanyika chini ya Serikali Kuu ambazo zilijumuisha ukaguzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na ukaguzi wa fedha za GAVI Aliance kwa ajili ya Chanjo ya Surua Rubella; Aidha, kaguzi zingine mbili zilifanyika chini ya Mashirika ya Umma ambayo ni ukaguzi wa Sekta ya Mafuta na Gesi na ukaguzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania.



YALIYOMO

UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI	i
DIBAJI	iii
SURA YA KWANZA	1
 1.0 UTANGULIZI	1
1.1 Wajibu na Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	1
1.2 Madaraka	2
1.3 Dira	4
1.4 Dhima	4
1.5 Misingi ya Uadilifu	4
1.6 Haki ya Mwananchi Kupata Taarifa.....	5
1.7 Taarifa za Ukaguzi	6
1.8 Rasilimali za Taifa na Uwajibikaji.....	6
 SURA YA PILI	8
 2.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI NA HATI ZA UKAGUZI	8
2.1 Aina ya Hati za Ukaguzi	8
2.2 Muelekeo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa.....	10

SURA YA TATU	11
3.0 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI	11
3.1 Matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za fedha za miaka ya nyuma	12
SURA YA NNE	15
4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU.....	15
4.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016	15
SURA YA TANO	25
5.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA	25
5.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa.....	25
SURA YA SITA.....	38
6.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA	38
6.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma..	38
SURA YA SABA.....	48
7.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA	48
7.1 Matokeo ya Ukaguzi	48



SURA YA NANE	56
8.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA UFANISI	56
8.1 Ukaguzi wa Usimamizi na Udhibiti wa Uchukuaji wa Maji kutoka katika Vyanzo vya Maji.....	56
8.2 Uendelezaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi	59
8.3 Usimamizi wa Samani za Barabara	61
8.4 Usimamizi wa Mikataba iliyoingiwa kati ya Serikali na Hospitali binafsi	64
8.5 Wahitimu wanaoanadaliwa kwenye Sekta ya Mafuta na Gesi Nchini	67
8.6 Usimamizi wa Kaguzi za Vyombo katika Usafiri wa Njia ya Maji	69
8.7 Uendelezaji wa Maeneo ya Wazi yalioainishwa Nchini	71
8.8 Usimamizi wa Usalama dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma	73
8.9 Ufutiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilifanyika na Kuwasilishwa Bungeni Mwaka 2012 na 2013	75
SURA YA TISA	78
9.0 RIPOTI YA KAGUZI MAALUMU	78
9.1 Ukaguzi wa Serikali Kuu	78
9.2 Mashirika ya Umma	80

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hii ndio taasisi kuu ya ukaguzi wa umma. Madaraka, Majukumu na Wajibu wa CAG yameainishwa kwenye katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyofanyiwa marekebisho) pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

1.1 Wajibu na Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtaka CAG kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa na Mfuko Mkuu wa Hazina, matumizi yake yameidhinishwa kulingana na idhini iliyotolewa na Bunge na kwa mujibu wa Ibara 136 na 140 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katiba inamtaka CAG kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha zote zilizoidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa kwa sheria iliyotungwa na Bunge na kwamba matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata mpango ulioidhinishwa.





CAG anapaswa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Serikali, Mahakama na Bunge.

1.2 Madaraka

CAG na kila mtumishi aliyeruhusiwa na yeye, atakuwa na haki ya kuchunguza vitabu, kumbukumbu na hati nyingine zote zinazohusika na kazi yake ya kikaguzi. Vilevile, CAG

atawasilisha kwa Rais kila taarifa ya ukaguzi atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 2 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, baada ya Rais kupokea taarifa hiyo Rais atawaagiza wahusika kuwasilisha taarifa hiyo ndani ya siku 7 kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa. Iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwa Spika au Naibu wake kwa kipindi kilichotajwa, CAG atachukua jukumu hilo yeye mwenyewe.

Kwa mujibu wa katiba Ibara ya 6 (2) (3) (4) CAG hatalazimika kutekeleza amri au maagizo ya mtu yeote au idara nyininge yoyote ya serikali. Mahakama nayo haitazuiliwa kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama CAG ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa katiba.

Pamoja na CAG kutoa ripoti kila mwaka ilionekana kwamba kuna ugumu kwa mwananchi wa kawaida kuisoma na kupata ujumbe uliokusudiwa katika ripoti hizo. Ni kutokana na sababu hiyo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuanzia mwaka 2013 ilianzisha utaratibu wa kutoa Toleo Maalum kwa ajili ya Wananchi ambalo limeandikwa kwa lugha rafiki, nyepesi na lugha ya picha ili kumwezesha mwananchi wa kawaida kupata taarifa za ukaguzi kupitia picha zilizotumika.

Ripoti ya kwanza toleo la mwananchi ilianza kusambazwa mwaka 2013, ambapo ripoti ya ukaguzi iliyosambazwa ilikuwa ya mwaka wa fedha 2011/2012. Ripoti ya pili ilisambazwa mwaka 2015 ikitoa ripoti ya Ukaguzi wa mwaka wa fedha



2012/2013. Aidha, ripoti ya tatu ya mwaka wa fedha 2013/2014 ilisambazwa mwaka 2016. Ripoti hii ni toleo la nne ambalo linawasilisha ripoti ya hesabu zilizokaguliwa zilizoishia tarehe 30 Juni 2016, Kaguzi Maalum na Kaguzi za Ufanisi.

1.3 Dira

Kuwa Taasisi ya hali ya juu katika ukaguzi wa sekta ya umma.

1.4 Dhima

Kutoa huduma za ukaguzi wa sekta ya umma zenye ubora wa hali ya juu zinazoimarisha utendaji, uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

1.5 Misingi ya Uadilifu

1.5.1 Kutopendelea - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.

1.5.2 Ubora - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaamu.

1.5.3 Uadilifu - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.

1.5.4 Zingatio kwa Wadau - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inalenga matakwa ya wadau kwa kujenga utamaduni wa kutoa huduma bora kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na ari ya kazi.

1.5.5 Ubunifu - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.

1.6 Haki ya Mwananchi Kupata Taarifa



Ibara 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweuka bayana kuwa taarifa ni haki ya mwananchi. Aidha, Sheria ya Kupata Taarifa Na. 6 ya mwaka 2016 na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 zimeweka utaratibu wa utoaji taarifa kwa misingi ya sheria.



Ofisi ya Taifa ya Ulagazi katika kutekeleza matakwa hayo iliamua kuja na Toleo maalum ambalo litamsaidia mwananchi kushiriki kikamilifu katika kuliletea Taifa lake maendeleo.

1.7 Taarifa za Ulagazi

Kwa mujibu wa kanuni ya 8 (5) ya kanuni za Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004); Wizara, Wakala na Idara za Serikali zina jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa kuhusu shughuli na rasilimali za taasisi husika zinatolewa kwa umma. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuandaa taarifa za mapato na matumizi yake kisha kila mwananchi kutafuta taarifa hizo ili kufuatilia utekelezaji wa shughuli za maendeleo nchini.

1.8 Rasilimali za Taifa na Uwajibikaji

Rasilimali za Taifa zinajumuisha fedha, maliasili ya nchi, watu, ardhi na mambo mengine yote yanayohitajika katika uendeshwaji wa Serikali kama ilivyoelezwa kwenye ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Uwajibikaji katika rasilimali za Taifa ni dhana ya maadili na utawala bora jukumu ambalo wanapewa watu au taasisi ili kuzilinda rasilimali za umma na kuwa tayari kuwajibika kwa maamuzi waliyoyafanya.

Kwa muundo wa Serikali Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna mihimili 3 ya uwajibikaji nchini ambayo ni Bunge, Serikali na Mahakama.

1.8.1 *Bunge*

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Wananchi lina wajibu wa kuidhinisha na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali. Wananchi kupitia wabunge wao wanaweza kutoa maoni yao ya namna ambavyo wangependa serikali iweze kutatua matatizo yao.

1.8.2 *Serikali*

Serikali inawajibu wa kukusanya na kutumia rasilimali za Taifa kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Serikali imegawanyika katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika na Taasisi za umma.

1.8.3 *Mahakama*

Mahakama ina wajibu wa kusikiliza mashauri yote yanayofikishwa mahakamani na kutoa hukumu kulingana na sheria za nchi.



SURA YA PILI

2.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI NA HATI ZA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana wajibu wa kukagua na kutoa taarifa ya ukaguzi wa Serikali na mashirika yake juu ya mapato na matumizi yake.

CAG anapotoa taarifa ya ukaguzi hutoa maoni ya kitaalamu ambayo huitwa hati. Maoni ya ukaguzi ni hati za ukaguzi zinazotolewa kwa mkaguliwa kama uthibitisho wa matokeo ya ukaguzi kwa upande wa ukaguzi wa taarifa za fedha tu. CAG hutoa maoni hayo kwa kuangalia iwapo mkaguliwa amezingatia viwango vya kimataifa vya taaluma ya uhasibu na vile vya Bodi ya Uhasibu Tanzania (NBAA).

2.1 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi ambazo hutolewa kutokana na mazingira tofauti anayokutana nayo mkaguzi. Aina hizo ni kama ifuatavyo:

2.1.1 Hati inayoridhisha

Hati hii hutolewa wakati matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi hazina makosa mengi na taarifa hizo zimezingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa sheria na kanuni.

2.1.2 Hati yenye Shaka

Hati yenye Shaka inafanana sana na hati inayoridhisha isipokuwa hati hii hutolewa pale ambapo taarifa za fedha zilizokaguliwa huonekana kuwa na makosa machache lakini zimezingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma pamoja na sheria na kanuni. Kwa kuwa matokeo ya ukaguzi huonesha mapungufu machache ambayo hayaathiri taarifa za fedha kwa ujumla, mkaguliwa hupewa Hati yenye Shaka ili kurekebisha mapungufu hayo.

2.1.3 Hati Isiyoridhisha

Hati Isiyoridhisha hutolewa wakati inapogundulika kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa na kukaguliwa kwa kiasi kikubwa zinakasoro kama vile kutozingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma wakati wa uandaaji wa taarifa hizo au kupuuza kwa matakwa ya kisheria na miongozo mbalimbali ya usimamizi wa masuala ya fedha.

Maelezo ya maeneo yenye mapungufu huoneshwa wazi na mkaguzi ili kumsaidia mkaguliwa kufahamu sababu zilizopelekea kupewa Hati Isiyoridhisha.

2.1.4 Hati Mbaya

Hati Mbaya hutolewa wakati taarifa za fedha zilizokaguliwa zinaonesha kuwa hazijakamilika hivyo kukosekana kwa uhuru au kuwepo kwa ufinyu mkubwa wa mawanda ya ukaguzi ambao husababishwa na mkaguliwa kwa makusudi au la.



2.2 Mwelekeo wa Hati za Uguzi zilizotolewa

2.2.1 Idadi ya kagazi zilizofanyika

Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2016, Mdhhibit na Mkagazi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alifanya jumla ya kagazi 222 kwa upande wa ukagazi wa Serikali Kuu; Mashirika ya Umma 112; Halmashauri 171; na Miradi ya Maendeleo 797.

2.2.2 Hati Zilizotolewa

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016; CAG ametoa jumla ya Hati za Uguzi 1302. Kati ya hati hizo Hati Zinazoridhisha ni 1161; Hati zenye Shaka 131; Hati Zisazoridhisha 5 na Hati Mbaya 5. Muhtasari wa hati zilizotolewa kwa mwaka huu, umeoneshwa kwenye Jedwali Na. 1.

Jedwali Na 1 : Muhtasari wa Hati zilizotolewa Mwaka 2015/2016

Na.	Taasisi zilizokaguliwa	Idadi ya Taasisi zilizokaguliwa	Aina ya hati za uguzi			
			Hati zinazoridhisha	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya
1.	Wizara, idara na Taasisi zake	222	190	24	3	5
2.	Halmashauri	171	138	32	1	0
3.	Mashirika ya Umma	112	108	4	0	0
4.	Miradi ya Maendeleo	797	725	71	1	0
Asilimia (%)			89.2%	10.1%	0.4%	0.4%

SURA YA TATU

3.0 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Sura hii inatoa taarifa ya ufuutiliaji wa mapendekezo mbalimbali ya ukaguzi wa fedha kwa miaka iliyopita ambapo inajumuisha taarifa za ukaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Miradi ya Maendeleo. Mapendekezo haya yalilenga kuimarisha usimamizi wa rasilimali za umma pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato.



Mapendekezo ya Ukaguzi yamegawanyika katika makundi matatu ya utekelezaji, yaani ya muda mfupi, ya muda wa kati na ya muda mrefu.



3.1 Matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za fedha za miaka ya nyuma

Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa miaka iliyopita kwa ujumla hauridhisih. Kati ya mapendekezo 234 yaliyotolewa ni mapendekezo 32 (14%) tu yametekelezwa kikamilifu. Mchangau wa utekelezaji wake umeainishwa katika Jedwali Na. 2

Jedwali Na 2: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa miaka iliyopita - 2012/13 na 2013/14

Na.	Aina ya Ripoti	Idadi ya Mapendekezo	Utekelezaji Umekamilika	Utekelezaji unaendelea	Utekelezaji Haujaanza
1.	Serikali Kuu	102	29	53	20
2.	Serikali za Mitaa	79	3	35	41
3.	Mashirika ya Umma	53	0	14	39
4.	Miradi ya Maendeleo	5704	1489	1527	2688
Jumla		5938	1521	1629	2788
Asilimia		100	26	27	47

Aidha, utekelezaji wa mapendekezo ulikuwa ni mbaya zaidi kwa Serikali za Mitaa kwani tathimini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi za miaka miwili ya fedha iliyopita (2012/13 na 2013/14) inaonesha kuwa kati ya mapendekezo 41 yaliyotolewa ni mapendekezo 16 (39%) utekelezaji wake unaendelea na mapendekezo 25 (61%) utekelezaji wake haujaanza kabisa.



Jitihada za serikali zinahitajika katika kuhakikisha kuwa mapendekezo yanayotolewa na CAG yanatekelezwa kikamilifu ili kuleta tija katika usimamizi wa rasilimali za umma.



RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU



KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2016

SURA YA NNE

4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha kwa taasisi 222 zilizokaguliwa zikiwemo Mafungu 62 ambayo hujumuisha Wizara na Taasisi; Hesabu Jumuifu za Taifa 1; Mamlaka ya Mapato Tanzania 1; Sekretarieti za Mikoa 25; Wakala wa Serikali 33; Mifuko Maalum 13; Balozi za Tanzania 34; Bodi na Mamlaka za Maji 13; taasisi nyinginezo 34; Vyama vya Siasa 5 na Kaguzi Maalumu 1.

4.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

4.1.1 Utekelezaji wa bajeti

Ukaguzi uliofanyika katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 ulibaini mapungufu katika ukukusanyaji wa mapato ambapo serikali haikufanikiwa kukusanya 6% ya makisio ya mapato¹. Aidha, ukaguzi ulibaini 7% ya fedha za matumizi ya kawaida na 24% ya fedha za maendeleo hazikupokelewa. Kukosekana kwa fedha hizi kumechangia kukwamisha baadhi ya shughuli za utendaji wa serikali ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Taarifa ya makusanyo imeoneshwa kwenye Jedwali Na. 3.

1 Mapato ya Kodi, yasiyotokana na kodi, mikopo ya ndani na nje pamoja na misaada ya wahisani



Jedwali Na. 3: Tofauti ya makisio na makusanyo halisi ya bajeti ya Serikali Kuu

Maelezo	Fedha za makusanyo ya mapato (Sh. Bilioni)	Fedha za matumizi ya Kawaida (Sh. Bilioni)	Fedha za matumizi ya Maendeleo (Sh. Bilioni)
Makisio ya Fedha	22,496	12,905	4,969
Fedha zilizokusanywa/ pokelewa	21,109	12,065	3,769
Fedha zisizokusanywa/ pokelewa	1,387	840	1,200
Asilimia ya fedha zisizokusanywa/pokelewa	6%	7%	24%

4.1.2 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa Hesabu Jumuifu (Hesabu za Taifa)

- i. Taasisi zinazofunga hesabu kwa tarehe tofauti zilijumuishwa kwenye uandaaji wa hesabu jumuifu bila ya kufanya marekebisho hali inayofanya taarifa hizo zisiwe sahihi. Mfano hesabu za taasisi za mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni zilichanganywa na hesabu za mwaka wa fedha unaoishia 31 Desemba. Kuna haja ya taasisi zote za umma kufuata mwaka mmoja wa fedha.

- ii. Kuna tofauti ya hesabu zilizopo kwenye vitabu vya taasisi husika na zile zilizopo kwenye vitabu jumuifu. Tofauti hii hutokana na kuingiza hesabu katika kitabu cha majumuisho kabla ya hesabu hizo kukaguliwa hivyo hupelekea hesabu hizo kutokuwa sahihi.

Mapendekezo: Serikali isimamie miongozo inayotolewa ili taasisi zote za umma zifunge hesabu sambamba na mwaka wa serikali na itumie taarifa zilizokaguliwa katika kufanya majumuisho.

4.1.3 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania

- i. Misamaha ya kodi yenyе thamani ya Sh. 3,455,008,267 ilitolewa kwa kampuni mbili (2) zilizoagiza magari 238 ambayo yalisajiliwa kwa kampuni nane (8) ambazo kati ya hizo ni kampuni moja tu iliyostahili kunufaika na msamaha huo. Hii inaonesha bado kuna matumizi mabaya ya misamaha ya kodi.
- ii. Mifumo mibovu ya kudhibiti mizigo katika bandari kavu za Tunduma na Kigoma imesababisha serikali kutokusanya kodi ya forodha ya Sh. 4,598,307,737 kwa mizigo 769 iliyohesabiwa kama mizigo ya kwenda nje ya nchi kumbe ilikuwa mizigo ya ndani.
- iii. Wafanyabiashara 8,165 kati ya 9,743 waliosajiliwa kulipa VAT hawakuwa na mashine za (EFD) kwa ajili ya kutoa risiti. Pia ukaguzi ulibaini kuwa katika mikoa mitano yenye wafanyabiashara 49,009 kati ya hao 36,882 hawana mashine



za EFD. Kutotumia mashine hizo kunazuia usimamizi mzuri wa mapato hivyo kutoa mianya kwa wafanyabiashara kukwepa kodi.

Mapendekezo: *Mamlaka ya Mapato Tanzania iimarishe udhibiti na usimamizi wa misamaha ya kodi na matumizi ya mashine za EFD.*

4.1.4 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa Deni la Taifa

- i. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 Deni la Taifa liliongezekwa kutoka sh. bilioni 33,540 (30 Juni 2015) hadi sh. bilioni 41,039 (30 Juni 2016) ongezeko la shs. bilioni 7,500 sawa na asilimia 22. Ukuaji wa Deni la Taifa linaweza kuleta athari katika utekelezaji wa shughuli za kawaida na maendeleo ya taifa kwa sababu sehemu ya mapato ambayo yanetumika kwa shughuli za maendeleo ya wananchi sasa yanatumika kulipa madeni hayo.
- ii. Hali ya uchumi na mazingira ya wakati wa kuanzishwa kwa sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada ya Mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2004) yamebadilika jambo linalosababisha changamoto katika usimamizi wa Deni la Taifa. Ipo haja ya kurekebisha Sheria zilizopo ili ziendane na hali ya sasa.

Mapendekezo: *Serikali iongeze juhudhi ya kukusanya mapato ili iongeze uwezo wa kuhudumia madeni na pia ipitie na kurekebisha muundo wa Usimamizi wa Deni la Taifa uliopo hivi sasa.*

4.1.5 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa awali wa malipo ya Pensheni yanayolipwa na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

- i. Wakati wa uhakiki wa malipo ya pensheni ilibainika kuwa majadala 274 yalizidishiwa sh. 1,120,442,386 na majadala 205 yalipunjwa sh. 595,863,986 zilizotokana na dosari za ukokotoaji hivyo kama CAG asingefanya ukaguzi wa awali Serikali ingepata hasara ya Sh. 524,578,400. Kutokuwepo kwa mifumo thabiti ya ndani ya udhibiti wakati wa uandaaji wa malipo ya pensheni ni mionganini mwa sababu zinazochangia katika ukokotoaji wa mafao yasiyo sahihi.

Mapendeleko: *Maafisa masuuli watoe mafunzo ya mara kwa mara kwa waandaaji wa mafao ya pensheni ili kuweza kuandaa mafao kwa kufuata kanuni na sheria za mafao.*

4.1.6 Mapungufu katika usimamizi wa Rasilimaliwatu na ulipaji wa mishahara

- i. Serikali ilipata hasara ya Sh. 1,242,203,804 kutokana na malipo ya mishahara kwa watumishi hewa 260 na sh. 50,525,058 ikiwa ni makato mbalimbali kwa watumishi hao.
- ii. Jumla ya watumishi wa umma 764 katika taasisi saba (7) hawakufanyiwa tathimini ya utendaji kazi. Hali hii inasababisha taasisi kutotambua mapungufu ya kiutendaji kwa watumishi wake ili kuweka mikakati ya kuyaondoa.



Mapendekezo: Serikali iendelee kufanya ukaguzi endelevu wa rasilimaliwatu ili kuhuisha orodha ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi wake pamoja na kuhakikisha utendaji wa watumishi wote wa umma unapimwa ili kuboresha uwajibikaji na utoaji huduma.

4.1.7 Mapungufu katika utendaji wa Wakala wa Serikali

- i. Kiasi cha sh. 523,929,676 kati ya Sh. 525,717,522 za michango kutoka halmashauri mbalimbali iliyokusudiwa kuanzisha Kitega Uchumi zilitumika kinyume na makusudio na bila idhini ya mukutano mkuu wa mwaka wa Shirikisho la Serikali za Mitaa (ALAT).
- ii. Licha ya muda wa marejesho kupita, kiasi cha sh. 1,345,206,622 (40%) kati ya Sh. 3,342,970,002 zilizotolewa na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) kama mikopo (mkopo pamoja na riba) kwa wateja mbalimbali katika wilaya za mkoa wa Dodoma hazikurejeshwa.
- iii. Mkopo wa Sh. 514,000,000 kutoka Mpango wa Taifa wa Uwezeshaji Kiuchumi (NEEP) kwenda kwenye Mfuko wa Rais wa Uwezeshaji zilitumika kwa masuala ya kiutawala badala ya masuala ya uwezeshaji.

Mapendekezo: Maafisa masuuli wa ALAT, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo na Mfuko wa Rais wa Uwezeshaji wanapaswa kuwajibishwa kwa matumizi mabaya ya fedha za umma.

4.1.8 Mapungufu katika usimamizi wa manunuzi na mikataba

- i. Thamani ya fedha ya sh. 3,452,112,838 haikuweza kuthibitika katika Taasisi nane (8) zilizofanya malipo kwa ajili ya bidhaa, kazi na huduma ambazo hazikupokelewa.
- ii. Taasisi kumi na tano (15) zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma yenyeye thamani ya Sh. 24,216,625,390 bila ushindanishi (nukuu za bei angalau tatu kutoka kwa wazabuni na wakandarasi).
- iii. Taasisi kumi (10) zilizokaguliwa zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma ya Sh. 11,253,346,373 na USD 29,606,100 bila ya kuwa na mikataba au makubaliano na wazabuni, suala ambalo halikubaliki kisheria.

Mapendekezo: *Taasisi za serikali zizingatie Sheria ya Manunuzi ya Umma ili kuepuka mapungufu yaliyojitekeza.*

4.1.9 Mapungufu katika usimamizi wa malipo

- i. Taasisi sita (6) zilifuja kiasi cha sh. 1,460,570,913.
- ii. Uhalali na uhalisia wa Sh. 91,347,958,833 kwa taasisi nane (8) zilizofanya malipo haukuthibitika kutohana na ukosefu wa nyaraka za malipo na viambatisho vyake.
- iii. Taasisi kumi na mbili (12) zilichepusha Sh. 3,830,032,676 na kuzitumia katika shughuli ambazo hazikuwepo kwenye bajeti.



Mapendekezo: *Taasisi za serikali zinatakiwa kuimarishe mifumo yao ya ndani kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Umma. Pia, hatua stahiki zichukuliwe kwa taasisi zote zilizoshindwa kuwasilisha hati za malipo na kuhakikisha fedha zinatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.*

4.1.10 Mapungufu katika usimamizi wa mali za kudumu na madeni

- i. Taasisi 69 hazikuwa na daftari lenye orodha ya mali za kudumu pamoja na thamani ya mali hizo.
- ii. Taasisi 11 hazikuwa na nyaraka za umiliki wa ardhi na majengo.
- iii. Taasisi 10 hazikuwa na alama za utambulisho kwenye mali zao ili kurahisisha mfumo wa ufuatiliaji, kuzuia wizi au upotevu wa mali za serikali.
- iv. Taasisi 92 zina malimbikizo ya madeni yanayofikia Sh. 1,979,323,563,821. Madeni haya yamejumuisha matibabu nje ya nchi, pango, watumishi na kesi ambazo hazijafanyiwa maamuzi. Kuna hatari ya serikali kuingia kwenye matumizi yasiyo na manufaa kwa umma kwa kulipa deni, faini pamoja na riba.

Mapendekezo: *Taasisi zinatakiwa kufanya mapitio ya mali zake kila mwaka ili kujua thamani za mali ambazo zitaoneshwa kwenye daftari la mali za kudumu pamoja na hesabu zao. Pia taasisi zinahimizwa kuwa na nyaraka za umiliki wa kisheria na ziweke*

alama za uthibitisho kwenye mali hizo. Vilevile, Serikali inatakiwa kulipa madeni yote yaliyohakikiwa, kutoa fedha kulingana na bajeti.

4.1.11 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa Vyama vyta Siasa

- i. Vyama vinne (NRA, UPDP, CHAUMMA na UMD) havikuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi.
- ii. Vyama vitatu (Demokrasia Makini, Chama cha Kijamii na ADC) havina akaunti za benki kama inavyotakiwa na Sheria Na.5 ya vyama vyta Siasa ya mwaka 1992 (Iliyorejewa 2015).

Mapendekezo: *Msajili wa Vyama vyta Siasa anatakiwa kuwawajibisha viongozi wa vyama vilivyoshindwa kutoa taarifa ya fedha kwa ajili ya ukaguzi na kuhakikisha vyama hivyo vinazingatia sheria.*



RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA



KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2016

SURA YA TANO

5.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA

Sura hii inatoa muhtasari na majumuisho kuhusu ukaguzi wa taarifa za Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) 171 zilizofanyika mwaka wa fedha 2015/2016.

5.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa

Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2016 ulibaini kasoro katika maeneo yafuatayo:

5.1.2 Utekelezaji wa bajeti

- i. Mamlaka za Serikali za Mitaa 139 hazikukusanya mapato ya ndani ya sh. 80,532,742,421 sawa na 21% ya Sh. 387,261,472,093 zilizokadiriwa. Hii inaonesha kwamba mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ziliandaa bajeti bila kufanya upembuzi yakinifu na pia mikakati ya ukusanyaji mapato haikuwa mathubuti.
- ii. Halmashauri 59 zilipokea Sh.144, 587,879,454 katika ruzuku ya matumizi ya kawaida ikiwa ni zaidi bajeti iliyoidhinishwa. Halmashauri ya **Wilaya ya Nyang'hwale** iliongoza kwa kuwa na zidio la 44%, Halmashauri ya **Wilaya Mlele** 41% na Halmashauri ya



- Manispaa Kigoma** 38%. Hii inaweza kuwa chanzo cha matumizi mabaya na ubadhirifu wa fedha za umma.
- iii. Mamlaka 20 za Serikali za Mitaa zilipokea fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha Sh.17,681,703,910 sawa na 24% zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa. Halmashauri ya **Wilaya ya Kibondo** iliongoza kupokea fedha takribani mara tatu na nusu ya fedha zilizoidhinishwa, ikifuatiwa na Halmashauri ya **Wilaya ya Kilolo** iliyopokea karibia mara tatu ya fedha iliyoidhinishwa na Halmashauri ya **Manispaa ya Ilala** mara mbili ya bajeti iliyoidhinishwa. Upelekaji wa fedha zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa ni ukiukwaji wa usimamizi wa bajeti
 - iv. Mamlaka za Serikali za Mitaa 151 hazikupokea fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha Sh.620,124,751,802 sawa na 61% pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa. Hii inaonesha kuwa kuna miradi ya maendeleo ambayo haikutekelezwa kabisa au ilitekelezwa kwa sehemu tu.

Mapendekezo: Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani. Aidha, Hazina itoe fedha kulingana na bajeti.

5.1.3 Usimamizi wa Rasilimaliwatu na mishahara

- i. Serikali ilipata hasara ya sh. 6,093,855,101 kutohana na malipo ya mishahara kwa watumishi hewa kwa halmashauri 108 kati ya 171 zilizokaguliwa na sh. 2,183,831,539 ikiwa ni makato mbalimbali kwa watumishi hao.

- ii. Mishahara isiyolipwa ya sh. 3,329,467,964 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 53 ilikosa uthibitisho wa urejeshwaji Hazina. Utaratibu huu unaweza kutoa nafasi kwa benki au hazina kutumia fedha hizi kwa manufaa yake kinyume na utaratibu.
- iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa 30 hazikuwasilisha makato ya kisheria ya Sh.1,123,229,274 kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Mamlaka zinazoongoza katika tatizo hili ni Halmashauri ya **Wilaya Ukerewe** (Sh. 164,192,191) ikifuatiwa na Halmashauri ya **Jiji Mbeya** (Sh. 87,449,222). Hii imesababisha gharama za ziada kama vile tozo na riba kwa halmashauri husika. Kwa mfano Halmashauri ya **Wilaya za Kondoa, Monduli na Urambo** zimepata adhabu ya tozo ya kiasi cha Sh. 1,033,536,058, Sh.33,750,300 na Sh.10,230,836 mtawalia kwa kuchelewesha michango yake LAPF.
- iv. Mamlaka 11 za Serikali za Mitaa zilitoa karadha (mkopo wa mshahara kwa watumishi) kiasi cha Sh.300,892,897 ambazo hazikurejeshwa kwenye mamlaka husika. Hii inaashiria kwamba kuna udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa utoaji na urejeshwaji wa karadha kwa watumishi.
- v. Watumishi 625 katika Mamlaka 33 za Serikali za Mitaa walipokea chini ya theluthi moja ya mishahara kutokana na marejesho ya mikopo yaliyochukua zaidi ya theluthi mbili katika mishahara yao kila mwezi. Hii hupunguza tija kwa mamlaka na ufanisi wa kazi kwa watumishi husika.



vi. Walimu wapya 639 katika Mamlaka 4 za Serikali za Mitaa walilipwa mshahara wa mwezi mmoja mara mbili kiasi cha shilingi milioni 152 kutokana na mawasiliano duni kati ya halmashauri na hazina . Aidha katika halmashauri ya wilaya ya Meru watumishi wawili walilipwa takriban shilingi million 22 kwa mwaka 2015/2016 kutokana na kuwa na cheki namba mbili tofauti.

Mapendekozo: Mamlaka zinazohusika na ajira zinatakiwa kufanya kazi kwa pamoja na kuhakikisha kwamba unakuwepo mfumo wa mrejesho ili kuondoa mapungufu ya ulipaji wa mishahara ya watumishi pamoja na kuzingatia Agizo la 41 (1) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

5.1.4 Usimamizi wa Mikataba na Manunuzi

- i. Mamlaka 36 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi ya bidhaa, huduma, kazi na ushauri za shilingi bilioni 2. 1 bila kufuata mchakato wa ushindani wa manunuzi. Hali hiyo inatia shaka kama kweli thamani ya fedha ilipatikana katika manunuzi hayo.
- ii. Mamlaka 20 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 nje ya Mpango wa manunuzi. Halmashauri tatu zilizoongoza ni Halmashauri ya **Manispaa ya Musoma** shilingi milioni 719, Halmashauri ya **Wilaya ya Maswa**, shilingi milioni 181 na Halmashauri ya **Wilaya ya Kyela** shilingi milioni 146. Kitendo hiki kinachochea kufanyika kwa manunuzi pasipo kuzingatia mpango na ushindani.

- iii. Mamlaka 27 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi ya shilingi bilioni 1.2 kutoka kwa wauzaji ambao hawakuidhinishwa na Wakala wa Ununuzi wa Umma (GPSA). Hii inaweza kusababisha uwezekano wa kununua huduma na bidhaa zisizoendana na thamani ya fedha.
- iv. Mamlaka 17 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi ya shilingi milioni 908 pasipo idhini ya Bodi ya Zabuni. Hali hii inaweza kusababisha thamani ya fedha isipatikane.
- v. Mamlaka 25 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi ya bidhaa zenye thamani ya shilingi milioni 790 bila kukaguliwa na Kamati ya Ukaguzi. Halmashauri zilizoongoza ni Halmashauri ya **Jiji la Arusha** shilingi milioni 150, Halmashauri ya **Mji wa Tunduma** shilingi milioni 148 na Halmashauri ya **Wilaya ya Nkasi** shilingi milioni 108. Hii inaweza kusababisha kufanyika manunuzi hewa au bidhaa zenye ubora hafifu kwa bei ya juu na ambazo haziendani na vigezo vilivyowekwa katika mkataba.
- vi. Mamlaka 25 za Serikali za Mitaa zilifanya malipo ya Matengenezo ya Magari yenye thamani ya takribani shilingi milioni 722 katika karakana binafsi pasipo kibali cha TEMESA. Halmashauri tatu zilizoongoza ni Halmashauri ya **Wilaya ya Geita** shilini milioni 67, Halmashauri ya **Wilaya ya Mpanda** shilingi milioni 62 na Halmashauri ya la **Jiji la Arusha** shilingi milioni 58. Hali hii inaweza kusababisha matengenezo na



- ukarabati wa magari ya serikali kufanya kwa ubora wa chini, bei ya juu au kutolandana na viwango vya matengenezo yanayohitajika.
- vii. Mamlaka 6 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi ya vifaa tiba yenyeye thamani ya takribani shilingi milioni 73 nje ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) bila uthibitisho wa kutokuwepo vifaa hivyo. Hii ni kinyume na Kanuni za Manunuzi ya Umma na inaweza kusababisha kupata vifaa hivyo kwa bei isiyolingana na thamani.
 - viii. Mamlaka 9 za Serikali za Mitaa ziliagiza na kulipia bidhaa zenye thamani ya takribani shilingi milioni 65 ambazo hazikupokelewa. Baadhi ya halmashauri zilizofanya malipo hayo ni Halmashauri ya **Mji wa Moshi** kwa shilingi milioni 17, Halmashauri ya **Wilaya ya Pangani** shilingi 13 na Halmashauri ya **Wilaya ya Kyerwa** shilingi 9.

Mapendekezo: *Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe zinangatia sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya umma ili kuepuka mapungufu yaliyojitekeza.*

5.1.5 Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma

- i. Malipo yenyeye nyaraka pungufu kwa thamani ya takribani shilingi bilioni 10 yalifanyika kwenye mamlaka 109 za Serikali za Mitaa. Hivyo uhalali wa malipo hayo kutokana na kukosekana kwa nyaraka muhimu haukuweza kuthibitika.

- ii. Malipo yenyе thamani ya takribani shilingi bilioni 3 katika mamlaka 37 za Serikali za Mitaa hayakuwa na hati za malipo pamoja na viambatisho vyake. Mifano ya halmashauri zenyе tatizo hili ni Halmashauri ya **Wilaya ya Gairo** iliongoza kwa shilingi milioni 886, Halmashauri ya **Wilaya ya Meatu** shilingi milioni 330 na Halmashauri ya **Wilaya ya Geita** shilingi milioni 326. Uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitika.
- iii. Mamlaka 112 za Serikali za Mitaa zilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenyе thamani ya takribani shilingi bilioni 16 bila kupatiwa stakabadhi za kieletroniki. Hii inaashiria kuwa halmashauri husika zinachangia wazabuni kukwepa kodi na kuikosesha Serikali mapato.
- iv. Mamlaka 32 za Serikali za Mitaa hazikukata kodi ya zuio yenyе jumla ya takribani shilingi milioni 326 kwenye malipo yaliyofanywa kwa wauzaji wa bidhaa na watoa huduma hivyo kupelekeea upotevu wa mapato ya Serikali.
- v. Mamlaka 21 za Serikali za Mitaa zilifanya malipo yasiyostahili ya takribani shilingi milioni 661; mfano posho kwa watu ambao sio watumishi wa Halmashauri na malipo ya sherehe ambazo kwa ujumla hazikuwepo kwenye bajeti za Halmashauri husika. Baadhi ya halmashauri zilizofanya malipo hayo ni Halmashauri ya **Wilaya ya Longido** shilingi milioni 188, Halmashauri ya **Wilaya ya Nzega** shilingi milioni 178 na Halmashauri ya **Wilaya ya Musoma** shilingi milioni 114.



- vi. Mamlaka 14 za Serikali za Mitaa zilifanya malipo batili yenye takribani shilingi milioni 565. Shilingi milioni 238 sawa na 42% ililipwa na Halmashauri ya Wilaya **ya Songea** yaliyojumuisha kulipa posho kwa Madiwani kwa shuguli moja mara mbili na posho kwa wafanyakazi ambaohawakushiriki katika shughuli husika. Halmashauri ya **Manispaa ya Kinondoni** ililipa kiasi cha takribani shilingi milioni 75 iliyojumuisha tozo ya ucheleweshaji wa fidia iliyotokana na kuvunja nyumba mbili za makazi.
- vii. Mamlaka 112 za serikali za mitaa zilibainika kuwa na usimamizi mbovu wa matumizi ya mafuta ya magari yenye thamani ya takribani shilingi billion 2.

Udhaifu huu umeonekana katika halmashauri 46 ambazo zilitumia mafuta yenye thamni ya takribani shilingi milioni 947 bila uthibisho, halmashauri 10 zilitumia mafuta yenye thamani ya shilingi milioni 92 kwenye magari binafsi, halmashauri 4 zilitumia mafuta kwa kiwango cha kati ya lita 2 hadi 5 kwa kilomita moja (Halmashauri ya **Wilaya ya Kiteto**, Halmashauri ya **Wilaya ya Pangani**, Halmashauri ya **Wilaya ya Rufiji / Utete** na Halmashauri ya **Wilaya ya Tunduru**) badala ya lita moja kwa kilomita sita wakati halmashauri 52 zilitumia mafuta yenye thamani ya shilingi milioni 692 bila kuingiza kwenye daftari la kumbukumbu za safari za magari.

- viii. Ukaguzi wa fedha za ruzuku mashuleneni (Elimu bure) ulibaini kuwa serikali haipeleki fedha kulingana na idadi ya wanafunzi walio katika shule husika, hakuna wahasibu wa kusimamia fedha hizo na Mamlaka za Serikali za

- Mitaa hazifanyi ufuatiliaji wa kutosha ili kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa miongozo inayotolewa kutokana na kukosekana kwa mawasiliano kati ya hazina na mamlaka za serikali za mitaa kuhusu fedha zilizopelekwa mashulenii.
- ix. Halmashauri 22 zilipokea ruzuku ya Elimu bure pungufu ya bajeti kwa kiasi cha takriban shilingi bilioni 2. Kiasi kilichopokelewa kutoka hazina kilikuwa shilingi bilioni 5 badala ya shilingi bilioni 7 zilizoidhinishwa kwenye bajeti. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa ni kama zinavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4.

Jedwali 4 Fedha za ruzuku za shule ya msingi na sekondari

Kundi	Bajeti iliyo-idhinishwa	Kiasi kilichopokelewa	Pungufu	% ya pungufu
Sekondari	3,424,442,511	2,664,461,856	759,980,655	22
Msingi	3,794,506,925	2,519,963,387	1,274,543,538	34
Jumla	7,218,949,436	5,184,425,243	2,034,524,193	28

- x. Ugaguzi uliofanyika kwa mamlaka 48 za serikali za mitaa ulibaini udanganyifu katika matumizi ya fedha za uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 2015. Kwa mfano, Halmashauri ya **Wilaya ya Mbogwe**, Chunya na Halmashauri ya **Mji Tarime** ziliwasilisha nyaraka za kughushi wakati Halmashauri ya **Mji Tabora** haikuwasilisha nyaraka zake kutokana na taarifa kuwa ziliteketea kwa moto



Mapendekezo: Mamlaka za Serikali za Mitaa zizingatie matakwa ya memoranda ya fedha ya serikali za mitaa pamoja na sheria za kodi. Aidha Wizara ya Elimu iimarishe mawasiliano na serikali za mitaa ili kuondoa mapungufu yaliyopo katika utoaji wa ruzuku ya elimu bure. Vilevile, mamlaka za serikali za mitaa zisimamie matumizi ya mafuta (diseli na Petroli). Pia, mamlaka za nidhamu zihakikishe kwamba fedha zilizotumika vibaya kwenye uchaguzi zinarejeshwa na maafisa waliotumia vibaya fedha hizo wanawajibishwa.

5.1.6 Usimamizi wa Mapato ya Serikali za Mitaa

- i. Vitabu 871 vya Makusanyo ya Mapato kutoka mamlaka 52 za serikali za mitaa havikuwasilishwa kwa ajili ya Ulaguzi. Halimashauri zilizoongoza katika tati zo hili ni Halmashauri ya **Wilaya ya Iramba** vitabu 178, Halmashauri ya **Wilaya ya Bumbuli** vitabu 91 na H/W Longido vitabu 74. Hali hii inaleta mashaka kuwa kuna uwezekano mkubwa wa wizi wa mapato ya Halmashauri.
- ii. Mawakala wa kukusanya mapato katika mamlaka 80 za serikali za mitaa hawakuwasilisha mapato ya takribani shilingi bilioni 6. Mfano wa halimashauri ni Halmashauri ya **Wilaya ya Sumbawanga** haikupokea shilingi bilioni 1, H/W Mbeya shilingi milioni 295 na Halmashauri ya **Wilaya ya Mpwapwa** shilingi milioni 231. Hali hii inaweza kusababisha halmashauri husika kuwa na upungufu wa mapato kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali.

- iii. Mamlaka 33 za serikali za mitaa hazikuwasilisha vielelezo vya kupeleka benki maduhuli ya shilingi milioni 762. Tatizo limebainika katika halmashauri za Gairo iliongoza kwa kiasi cha shilingi milioni 195, Kinondoni shilingi milioni 99 na Misungwi shilingi milioni 51. Kukosekana kwa taarifa hizi kunatia shaka juu uhalali, usahihi na ukamilifu wa kiasi cha mapato ya ndani kilichkusanya.
- iv. Kiasi cha takribani shilingi bilioni 7 hazikurudishwa kwa Halmashauri husika na takribani shilingi milioni 314 kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo ni 30% ya makusanyo ya kodi ya matumizi ya ardhi kinyume cha mkataba. Hali hii hupunguza morali kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia ukusanyaji kodi ya matumizi ya ardhi.

Mapendekezo:

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuimarisha udhibiti wa ukusanyaji wa mapato ya ndani. Wizara husika inashauriwa kuharakisha marekebisho ya makubaliano ili mamlaka za Serikali za Mitaa ziwasilishe 70% tu za makusanyo ili kuepuka deni kubwa linaloendelea kukua.

5.1.7 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayogharamiwa kwa Fedha za Ndani

- i. Miradi yenye thamani ya takribani shilingi milioni 15 ilikuwa haijaanza kutekelezwa katika mamlaka 14 za Serikali za Mitaa licha ya fedha kuwepo kwa ajili



- ya miradi hiyo. Hii inaweza kusababisha kupanda kwa gharama za utekelezaji wa miradi husika.
- ii. Miradi yenye thamani ya takribani shilingi milioni 971 iliyokamilika katika mamlaka 11 za serikali za mitaa ilikuwa haijaanza kutumika. Kutotumika kwa miradi iliyokamilika kunawanyima wananchi fursa ya kupata huduma.
 - iii. Kiasi cha takribani shilingi milioni 29 katika halmashauri 151 sawa na 10% ya mapato ya ndani hazikingizwa kwenye mfuko wa wanawake na vijana. Kutochangia katika mfuko huo kunawanyima vijana na wanawake fursa ya kukopa na kupata mitaji ya kufanya shughuli mbalimbali kwa ajili ya kujiongezea kipato na hivyo kutofikiwa kwa malengo ya mfuko.
 - iv. Kiasi cha takribani shilingi bilioni 6 katika Mamlaka 59 za Serikali za Mitaa ambazo ni sawa na 20% ya Ruzuku ya Fidia ya Vyanzo vya ndani hazikuwasilishwa katika Vijiji. Hii ina maana kwamba shughuli za maendeleo katika ngazi za vijiji hazikutekelezwa kama zilivyopangwa.

Mapendekezo: Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuchukua hatua stahiki za usimamizi wa miradi iliyokamilika na isiyotelezwa katika ngazi zote. Aidha, mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe 20% ya ruzuku isiyokuwa na masharti iliyopokelewa kutoka Serikali Kuu inawafikia walengwa kwa wakati. Vilevile, Serikali iipitie upya na kuboresha Sheria inayosimamia utaratibu wa usimamizi wa agizo la 10% kupelekwa kwenye mfuko wa vijana na wanawake.



RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA



KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2016

SURA YA SITA

6.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA

Ripoti ya ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma inahusu ukaguzi wa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2016. Ripoti hii imeainisha masuala yanayoathiri mikakati na ufanisi wa utendaji wa Mashirika na Taasisi katika kutekeleza na kufanikisha malengo waliyojiwekea.

6.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma

Katika ukaguzi wa hesabu za Mashirika na Taasisi za Umma mapungufu mbalimbali yaliyobainika ni kama ifuatavyo:

6.1.1 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) ulitoa mkopo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya cha Chuo Kikuu cha Dodoma kiasi cha Shilingi bilioni 44.29 pasipo mkataba na uthhibitisho wa udhamini kutoka serikalini. Hali hii inasababisha kukosekana kwa uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma.

Mapendekezo: *NHIF ihakikishe inaingia mkataba wa mkopo kati yake na mkopaji. Pia NHIF ihakikishe haitoi tena mkopo wowote kabla ya kusaini mkataba.*

6.1.2 Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

Kiasi cha shilingi bilioni 1 kilichotolewa kwa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kwa dhamana ya serikali haikurejeshwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) licha ya muda wake kupita (tarehe 30 Juni 2015). Kushindwa kwa Serikali kuilipa NHIF kunadhoofisha uwezo wa mfuko katika kuwahudumia wanachama wake.

Mapendekozo: *NHIF ichukue hatua kuhakikisha Serikali inarejesha fedha hizo.*

6.1.3 Benki ya Wanawake Tanzania (TWB)

- i. Mikopo yenye jumla ya Shilingi milioni 655 ilitolewa kwa kampuni nne bila uthibisho wa uwepo wa kampuni hizo kwa msajili wa kampuni (BRELA).
- ii. Mkopo wa shilingi milioni 200 uliotolewa kwa mteja mmoja kwa mwaka wa fedha 2014/15 bila kuwa na dhamana iliyowekwa tofauti na miongozo ya utoaji mikopo.
- iii. Mikopo ya shilingi milioni 355 imetolewa kwa wateja sita (6) ambao leseni zao zimemalizika muda wake.
- iv. Mtaji wa benki ulikuwa chini ya kiwango kinachohitajika cha shilingi bilioni 5 kwa miezi 6 (Januari, februari, septemba, Oktoba, Novemba na Desemba 2015) kinyume na matakwa ya Kanuni na. 5 ya Kanuni za Benki na Taasisi za Fedha.



Mapendeleko: TWB *iimarishe udhibiti katika utoaji mikopo kwa kuhakikisha hatua zote muhimu zinafuatwa kabla ya uidhinishaji na utoaji wa mikopo ili kulinda maslahi ya benki na kuepusha udanganyifu unaoweza kufanywa na wakopaji pamoja na kufuatilia mwenendo wa mtaji kila siku na kuchukua hatua thabiti kudumisha kiwango cha chini cha mtaji.*

6.1.4 Shirika la Posta Tanzania (TPC)

- i. Hesabu za mwaka wa fedha 2014/15 za shirika zilionesha Shirika linaidai Serikali takribani shilingi bilioni 4 zilizokopwa kwa ajili ya kulipa pensheni ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Kuwepo kwa madeni, kukosekana kwa mipango ya kimkakati ya kibashara na miundombinu duni ya huduma ya Posta ni mionganoni mwa mambo yaliyochangia biashara kudorora.
- ii. Shirika limeshindwa kulipa takribani shilingi bilioni 1 kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA). Deni hilo linajumuisha ada ya mwaka na mirahaba kwa miaka iliyopita. Kushindwa kuzingatia sheria na kanuni kwa kulipa mirabaha na ada kama inavyotakiwa, TCRA inaweza kuwapa adhabu au kusimamisha leseni ya biashara.

Mapendeleko: Serikali irejeshe kiasi cha fedha ilichokopa pia Shirika lifanye mabadiliko makubwa ya kimkakati yenye kulenga kuimarisha ufanisi kwa watumishi na tija

kwenye biashara. Vilevile, shirika lifuate sheria, kanuni na taratibu zote na kuhakikisha kwamba deni lote linalipwa kwa Mamlaka(TCRA).

6.1.5 Tatizo la Uendelevu wa Benki ya Twiga

Benki ilipata hasara ya takribani shilingi bilioni 13 na upungufu wa mali ya wana hisa (Equity) wa takribani shilingi bilioni 21 kwa mwaka wa fedha ulioishia 31 Desemba 2014, pia ilipata hasara ya takribani Shilingi bilioni 3 na upungufu wa mtaji kwa wana hisa wenye thamani ya takribani shilingi bilioni 19 kwa mwaka wa fedha ulioishia 31 Desemba 2015. Aidha, mtaji wa msingi wa benki katika miaka miwili (2014 na 2015) ulikuwa chini ya kiwango cha chini cha shilingi bilioni 5 kwa mujibu wa sheria ya benki na taasisi za fedha. Hii inaathiri utendaji wa benki ambapo inaweza kupelekea kushindwa kuhudumia wateja wake.

Mapendekozo: *Benki ifanye tathimini ya kina na kuainisha sababu za kufanya vibaya pamoja na kubuni mikakati ya kuleta ufanisi.*

6.1.6 Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)

Katika mwaka wa masomo 2015/16 wanafunzi 3920 (78%) kati ya 5009 walishindwa katika mitihani ya muhula wa kwanza. Kwa mujibu wa mkutano wa 107 wa bodi ya uongozi wa chuo mojawapo ya sababu za wanafunzi kufeli ni utoro wa walimu na wanafunzi ambao umefikia kiasi cha asilimia 82.



Mapendekezo: *Bodi ichukue hatua stahiki na za haraka ili kutatua tatizo la utoro.*

6.1.7 Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)

- i. Kutokana na mikataba ambayo Shirika la umeme limeingia na kampuni binafsi za kuzalisha umeme imelisabishia shirika hasara ya Shilingi 265.3 kwa kila uniti inayouza. Bei ya kununua umeme kutoka kwa kampuni binafsi ni shilingi 544.65 na kuza shilingi 279.35 kwa kila uniti.
- ii. Deni la shirika la umeme kwa wateja binafsi na serikali hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2016 lilikuwa takribani shilingi bilioni 215, serikali inadaiba shilingi bilioni 145 Sawa na 67% ya deni lote na shilingi bilioni 70 sawa na 33% ni kutoka kwa wateja binafsi.

Mapendekezo: *Shirika litafute vyanzo mbadala vya umeme vyenye bei nafuu kama maji, gesi, umeme wa jua na upopo ili kuachana na wazalishaji binafsi wanaotumia mafuta. Aidha, mikataba ya ununuzi wa umeme kutoka wazalishaji binafsi iangaliwe upya. Serikali na taasisi zake zihakikishe zinalipa deni zinalodaiwa. Vilevile, TANESCO ichukue hatua madhubuti kukusanya madeni kutoka kwa wateja binafsi.*

6.1.8 Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

Kiwango cha utumikaji majengo 9 ya uwekezaji ya shirika la hifadhi ya jamii (NSSF) ni kati ya asilimia 0 mpaka 43 ilikilinganishwa na kusudio la kiwango cha chini cha kusudio la soko cha asilimia 80.

Mapendekezo: *Shirika liendelee kutangaza uwepo wa nafasi za kupangisha katika majengo yao. Aidha, ipo haja ya kufanya upembuzi yakinifu kuhusu uwepo wa soko la uhakika lenye kuwiana na nafasi zinazopatikana kwenye majengo ya vitega uchumi.*

6.1.9 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Licha ya kuwepo kwa Mtambo wa Kielektroniki wa Kufuatilia Mawasiliano (TTMS) hadi sasa TCRA haina mfumo (moduli) wenyewe uwezo wa kutambua na kufuatilia taarifa za matumizi ya intaneti na muda wa maongezi ili serikali iweze kupata mapato stahiki hivyo kupata hasara kwa kukosekana kwa ufuatiliaji wa taarifa za matumizi ya intaneti na muda wa maongezi.

Mapendekezo: *TCRA na TRA ambao ndio walengwa wakuu washirikiane kuhuisha moduli ya kudhibiti mapato ya ndani yatokanayo na matumizi ya intaneti na muda wa maongezi.*



6.1.10 Ukaguzi wa Sekta ya Madini

- i. Serikali imepata hasara kutoka kwenye migodi mikubwa minne (4) ya dhahabu na mmoja wa almasi kwa kipindi cha kat i ya Mwaka 2012 mpaka 2016 ya takribani shilingi trioni 1. Hii ni kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani iliyoruhusu tozo ya kodi kwa kiwango cha sifuri kwa bidhaa zinazosafirishwa kuuzwa nje ya nchi kwa lengo la kukuza viwanda vya ndani ambayo haikuonesha makundi ya bidhaa zipi zinastahili motisha hiyo.
- ii. Serikali imeshindwa kuhakiki gharama za uwekezaji za kampuni kubwa za madini ili kujuu gharama halisi za uwekazaji ambazo hupunguzwa kwenye mapato ya uzalishaji. Hali hii imesabisha ukosefu wa mapato kwa serikali ambapo kampuni kubwaa za madini zimekuwa hazilipi kodi kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2011 mpaka 2015 kwa kuonesha kwamba zinajijendesa kwa hasara.

Mapendekezo: Serikali ipitie upya Sheria hiyo ili kuondoa tozo ya kiwango cha sifuri kwenye mauzo ya madini na vito nje ya nchi na kuondoa kasoro zilizobainika. Vilevile, ihakiki gharama za uwekezaji na viwango vya uzalishaji katika migodi ili kuzuia udanganyifu.

6.1.11 Ubia kati ya STAMICO na TML

Licha ya kuwepo kwa kifungu cha 15.1(b-d) cha makubaliano ya ubia kati ya STAMICO na TML ambapo mionganini mwa mambo mengine TML na STAMICO wanapaswa kutafuta masoko ya Tanzanite kwa pamoja, imebainika kuwa TML hufanya kazi ya kutafuta masoko peke yake. Hii inatia shaka kama STAMICO imefanya jitihada yoyote ya kushirikiana na mbia mwenza TML kutafuta masoko.

Mapendekizo: *Wizara ya Nishati na Madini kupitia STAMICO isimamie mauzo ya Tanzanite ili kuhakikisha kuna uwazi katika minada ya hadhara na kuondoa mianya ya madini haya kuuzwa kwa bei isiyo ya ushindani kati ya kampuni tanzu.*

6.1.12 Mapungufu katika Mikataba ya uchimbaji Madini

Serikali iliingia mikataba isiyolinda maslahi ya umma kwa kampuni za madini ikiwemo Geita Gold Mining (GGM) inayoendesha mgodi wa dhahabu wa Geita, na Kampuni ya ACACIA inayoendesha migodi ya Buzwagi, Bulyanhulu na Mara Kaskazini. Kwa kuweka sera zisizoridhisha kwenye fedha za kigeni na forodha, vifungu vya sheria vinavyozua mabadiliko kwenye mikataba husika, motisha za kodi zilizozidi kwenye taratibu za kihasibu katika kutambua na kutohoa matumizi ya mitaji, serikali kutegemea taarifa za uvumbuzi na upembuzi zilizofanywa na makampuni binafsi



yanayoomba leseni bila kuwa na njia mbadala ya kuhakiki taarifa hizo zimechangia kuipunguzia serikali uwezo wa kutetea maslahi ya umma.



Miongoni mwa sababu zinazo ikosesha Serikali mapato kwenye sekta ya madini

Mapendeleko: Serikali itumie kifungu kinachoruhusu kurejewa kwa mikataba kinachopatikana kwenye mikataba mingi ya madini ili kuzingatia maslahi ya Taifa. Vile vile, iboreshe usimamizi wa kampuni binafsi zinazofanya kazi za kutafuta na kuvumbua miamba yenye madini ili kuwa na taarifa sahihi na za ziada zitakazoisaidia kwenye majadiliano na kufanya maamuzi.

RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO



KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2016

SURA YA SABA

7.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO

Sura hii inahusu muhtasari wa majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2016. Miradi ambayo inajumuisha miradi mikubwa minne inayofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wahisani kupitia mfuko wa pamoja na mfuko wa barabara ambao huchangiwa na chanzo cha mapato ya ndani yatokanayo na kodi ya mafuta. Miradi minne ya maendeleo ambayo huchangiwa kwa pamoja ni Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Afya (HBF), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), na Programu ya Maendeleo Sekta ya Maji (WSDP). Aidha, ukaguzi umefanyika katika miradi mingine inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa (UN) na Wadau wengine wa maendeleo.

7.1 Matokeo ya Ukaguzi

7.1.1 Masuala ya Usimamizi wa Bajeti

- i. Watekelezaji 40 wa miradi 3 walifanya matumizi ya takriban shilingi milioni 541 bila kutumia vifungu vilivystahili kufanya matumizi hayo. Miradi hiyo ni HBF ambapo watekelezaji 17 walitumia shilingi milioni 149, mradi wa RF watekelezaji 11 walitumia shilingi milioni 120 na mradi wa WSDP watekelezaji 12 walitumia shilingi milioni 272. Kufanya malipo kwa kutumia vifungu visivyostahili kunaathiri utekelezaji wa shughuli za miradi zilizopangwa.

- ii. Watekelezaji 33 wa miradi minne walitumia takriban shilingi milioni 932 zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa. Matumizi nje ya bajeti iliyoidhinishwa yalifanyika kama ifuatavyo; watekelezaji 15 katika mradi wa HBF shilingi milioni 318, kwenye mradi wa RF watekelezaji 9 shillingi milioni 361, mradi wa WSDP watekelezaji 8 shilingi milioni 153 na mtekelezaji mmoja wa TASAF shilingi milioni 100.
- iii. Watekelezaji 277 wa miradi minne hawakupokea shilingi bilioni 132 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Miradi hiyo ni: RF shilingi bilioni 51 hakikupokelewa na watekelezaji 112, ASDP shilingi bilioni 32 kwa watekelezaji 82, WSDP shilingi bilioni 46 kwa watekelezaji 79 na HBF shilingi bilioni 3 kwa watekelezaji 4. Kutokupokelewa kwa fedha hizo kunakwamisha kufikiwa kwa malengo ya miradi iliyokusudiwa kutekelezwa.
- iv. Malipo ya takriban shilingi milioni 453 yalifanywa na watekelezaji 23 wa miradi mitatu kwa ajili ya kulipia madeni kinyume na matakwa ya mradi. Kiasi cha shilingi milioni 220 kililipwa kwenye mradi wa RF na watekelezaji 6, shilingi milioni 141 kwenye mradi wa HBF wenye watekelezaji 14 na kiasi cha shilingi milioni 92 kwa watekelezaji watatu 3 wa mradi wa WSDP. Kutohana na malipo haya, kazi zilizoainishwa kwenye bajeti ya kila mradi hazikutekelezwa hivyo kuathiri malengo ya mradi.
- v. Watekelezaji 40 wa miradi mitano walichelewa kupokea shilingi bilioni 21 kutoka Hazina. Katika mradi wa ASDP watekelezaji 17 takriban shilingi bilioni 10, mradi wa



HBF shilingi bilioni 9, mradi wa RF watekelezaji 6 shilingi milioni 811, Mradi wa WSDP watekelezaji 4 shilingi milioni 610; na na mradi wa TASAF watekelezaji 13 shilingi milioni 203. Ucheleweshaji huo umeathiri utekelezaji na ukamilishaji wa miradi, vilevile hali hii husababisha watekelezaji wa miradi kuwa na bakaa kubwa mwisho wa mwaka.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi iliookusudiwa na watekelezaji wa miradi wahakikishe kazi zinatekelezwa kama zilivyoidhinishwa kwenye bajeti za miradi husika.

7.1.2 Mapungufu katika usimamizi wa fedha

- i. Watekelezaji 210 walifanya malipo ya takriban shilingi bilioni 11 kwenye miradi mitano bila ya kuwasilisha hati za malipo pamoja na viambatisho vyake. Hivyo, ni vigumu kuthibitisha kama malipo haya yalikuwa stahiki na halali. Malipo haya yalihuisha mradi wa RF watekelezaji 44 takriban shilingi bilioni 4, mradi wa WSDP watekelezaji 59 shilingi bilioni 3, mradi wa HBF watekelezaji 63 shilingi bilioni 2, mradi wa TASAF watekelezaji 39 shilingi bilioni 2 na mradi wa ASDP watekelezaji 5 shilingi milioni 20.



- ii. Ucheleweshaji wa urejeshaji wa masurufu ya takribani shilingi milioni 114 kwa zaidi ya mwaka yaliyotolewa kwa watumishi ni kinyume na Agizo 40(3) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 2009. Masurufu hayo yalikuwa ni kwa miradi ya WSDP shilingi milioni 74, HBF shilingi milioni 23 na RF shilingi milioni 17. Ukiukwaji huu unaashiria fedha kutotumika kwa shughuli zilizohusiana na miradi na pia kunasababisha kutojulikana matumizi halisi ya mradi katika mwaka husika.



- iii. Watekelezaji 290 wa miradi mitano walifanya manunuzi ya takriban shilingi bilioni 43 kutoka kwa wazabuni mbalimbali. Hata hivyo walishindwa kuwasilisha stakabadhi za kielektroniki wakati wa ukagazi kinyume na Kanuni Na. 10(5) na 29(1) ya sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani na Tamko la Serikali Na. 192 la tarehe 29 mei, 2010. Manunuzi hayo yalifanya kwenye miradi ya RF watekelezaji 92 shilingi bilioni 25, WSDP watekelezaji 74 shilingi bilioni 14, HBF watekelezaji 82 shilingi bilioni 3, TASAF watekelezaji 36 shilingi bilioni 1 na ASDP watekelezaji 6 shilingi milioni 188. Taasisi kushindwa kudai na kupata stakabadhi za kielektroniki zinawasaidia wamiliki wa biashara husika kukwepa kodi.

Mapendekizo: *Maafisa Masuuli waimarishe udhibiti wa ndani kwenye malipo na uresheshaji wa masurufu. Vilevile, wahakikishe wanapofanya manunuzi wanadai na kupewa stakabadhi za kieletroniki.*

7.1.3 Manunuzi na usimamizi wa mikataba

- i. Manunuzi ya vifaa na huduma kwa yenyewe thamani ya shilingi milioni 269 yalifanya katika Halmashauri 9 zilizotekeleza mradi wa HBF bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni.
- ii. Manunuzi ya shilingi milioni 770 yalifanya bila kushindanisha wazabuni katika Halmashauri 27 zilizotekeleza miradi mitatu ikiwemo WSDP shilingi milioni 422, HBF shilingi milioni 262 na TASAF shilingi milioni 86.

- iii. Kiasi cha shilingi milioni 160 kilitumiwa na halmashauri 15 kufanya manunuzi ya mali, kazi za ujenzi na zisizo za ushauri toka kwa Wazabuni wasioidhinishwa na Wakala wa Manunuzi ya Serikali (GPSA), ambapo shilingi milioni 110 zilitumika kwenye mradi wa HBF, shilingi milioni 32 mradi wa TASAF na shilingi milioni 17 mradi wa WSDP.
- iv. Halmashauri 14 zilizotekeleza mradi wa HBF zililipia bidhaa mbalimbali zenyе thamani ya shilingi milioni 120 bila ya bidhaa hizo kupokelewa na halmashauri husika.
- v. Mali na Vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 699 vilinunuliwa na watekelezaji wa miradi kwenye halmashauri 45 na havikuingizwa kwenye daftari la kutunza kumbukumbu za mali na vifaa. Mali na vifaa hivyo vilikuwa vya miradi ya HBF shilingi milioni 521, WSDP shilingi milioni 133 na mradi wa RF shilingi milioni 44.

Mapendekezo: *Maafisa Masuuli, Bodii za Zabuni na vitengo vya manunuzi vihakikishe manunuzi ya bidhaa na huduma yanafuata taratibu za manunuzi kwa mujibu wa sheria.*

7.1.4 Hoja za Miradi Mingine

- i. Ghala la Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ilihifadhi dawa ziliyokwisha muda wake zenyе thamani ya shilingi bilioni 10 zaidi ya miaka 12 badala ya kuteketeza dawa hizo. Hali hii imeongeza gharama za uhifadhi wa dawa na ni hatari kwa afya na mazingira.



- ii. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeshindwa kuchangia mchango wake wa takriban shilingi bilioni 4 sawa na asilimia 5.6 ikiwa ni gharama za kutoa mizigo, kuhifadhi na kusambaza dawa na vifaa tiba. Hii ni kinyume na mkataba ulioingiwa baina ya Bohari kuu ya Madawa (MSD) na Wizara. Hali hii inazorotesha utekelezaji wa mipango ya Bohari katika kutoa huduma mbalimbali.

Mapendekozo: *MSD ihakikishe inateketeza dawa pindi muda wake wa matumizi unapoisha. Vilevile, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipe sehemu ya gharama yake inayopaswa kuchangia kwa MSD ili iweze kutoa huduma zake ipasavyo.*

RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI



KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 MACHI 2017

SURA YA NANE

8.0 RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI

Sura hii inatoa taarifa ya kaguzi tisa za ufanisi zilizofanyika kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2017.

Madhumuni ya ukaguzi wa ufanisi ni kutoa tathmini ya kiwango ambacho thamani ya fedha yaani uwekevu, tija na ufanisi huzingatiwa na taasisi za serikali zinapotumia rasilimali katika kutekeleza majukumu yake. Maeneo ya kufanya ukaguzi wa ufanisi hubainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali ikiwemo malalamiko kutoka kwa wananchi au umuhimu wa eneo husika kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka huu ripoti za kaguzi za ufanisi zilizowasilishwa bungeni ni kama ifuatavyo:

8.1 **Ukaguzi wa Usimamizi na Udhibiti wa Uchukuaji wa Maji kutoka katika Vyanzo vya Maji**

Ukaguzi huu unahusu usimamizi na udhibiti wa uchukuaji wa maji kutoka kwenye vyanzo vya maji ambapo mabonde manne ya maji yalihusika ambayo ni Wami/Ruvu, Ziwa Viktoria, Pangani na Bonde la Kati. Kwa mujibu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria Na. 11 ya Mwaka 2009 kuhusu usimamizi wa Rasilimali za Maji zinaelekeza uzingatiaji wa uwepo wa mizania ya maji na akiba ya maji kwa ajili ya mazingira suala ambalo kwa sasa halizingatiwi katika utoaji wa vibali jambo ambalo linasababisha migogoro baina ya watumia maji wa juu na wa chini.

8.1.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kubaini ukubwa wa tatizo la uhaba wa maji unaotokana na uharibifu wa vyanzo vyta maji hivyo kusababisha migogoro kwa watumiaji wa maji.

Kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi, waheshimiwa wabunge, vyombo vyta habari na taasisi mbalimbali zisizo za kiserikali juu ya uharibifu wa vyanzo hivyo CAG aliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi katika eneo hili ili kutafuta ufumbazi wa kudumu wa tatizo hilo.

8.1.2 Mapungufu yaliyobainika

- i. Hakukuwa na mpango jumuifu wa usimamizi wa rasilimali za maji katika mabonde hayo kwa kuwashirikisha wadau wote. Hii ilisababisha utoaji wa vibali pasipo kuzingatia kiasi cha maji kinachopatikana katika mabonde hayo.
- ii. Hakukuwa na udhibiti kwa watumiaji wa maji. Kukosekana kwa udhibiti kulisababisha kuzidisha viwango vyta uchukua jwa maji tofauti na ilivyoainishwa kwenye vibali vyao. Mfano, MWAUWASA ilizidisha maji kwa asilimia 70 (ilitumia mita za ujazo 90,000 badala ya 53,000 kwa siku) ambapo iliikosesha mapato Bodi ya Bonde kiasi cha takribani shilingi milioni 41 kama malipo ya ziada kutoka kwa watumiaji waliozidisha viwango vyao.



- iii. Bonde la maji la Ruvu limepoteza mapato ya takriban shilingi milioni 814 kutokana na visima vilivyochimbwa katika wilaya ya llala pekee bila kufuata utaratibu rasmi na hivyo kutotambuliwa na Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu. Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya visima 2888 vilivyopo wilayani llala ni visima 262 pekee ndio vipo kwenye orodha ya usajili.
- iv. Kumekuwapo na udhaifu katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ada wanazolipa wenyе vibali vya kuchukua maji katika mabonde. Mabonde manne yalikosa takribani shilingi bilioni 2 sawa na 40% ya kiasi cha shilingi bilioni 5 walizotakiwa kukusanya katika kipindi cha miaka 5 (2011/2012 hadi 2015/2016). Mfano DAWASCO anadaiwa takribani shilingi milioni 869 na Bonde la maji la Wami/Ruvu. Udfaifu wa ukusanyaji wa mapato umesababisha wenyе vibali vya kuchukua maji katika mabonde hayo kutofuata sheria na makubaliano waliyoingia baina yao na mamlaka za mabonde. Hali hii imechangia Bodi za Mabonde kukosa fedha za kutekeleza baadhi ya majukumu yao.

Mapendekezo: *Wizara ya Maji na Umwagiliaji iyaagize mabonde kuzigatia matumizi endelevu katika vyanzo vya maji, hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa kunakuwapo na mpango wa pamoja wa usimamizi rasilimali maji unaotumika katika mabonde yote. Aidha, udhibiti uimarishwe katika ukusanyaji wa mapato pamoja na wachukuaji wa maji wasio na vibali na wale wanaozidisha viwango vilivyoainishwa katika vibali vyao.*

8.2 Uendelezaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi

Ukaguzi huu unahu su uendelezaji wa Miundo mbinu ya shule za msingi nchini. Kwa muda mrefu sasa kumekuwapo na malalamiko toka kwa wananchi, wabunge na vyombo nya habari kuhusu kuwepo kwa uhaba na miundombinu duni katika shule za msingi. Hali hii inasababisha kutokuwepo mazingira rafiki kwa mwanafunzi kujifunza na hivyo kuchangia kushuka kwa kiwango cha elimu.

8.2.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kubaini kama Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI wametekeleza ipasavyo jukumu la kuhakisha kama kuna miundo mbinu ya kutosha na rafiki kwa shule za msingi yenye kuwezesha uwepo wa mazingira rafiki ya kujifunzia kwa wanafunzi.

8.2.2 Mapungufu yалиyobainika

- i. Mahitaji ya msingi katika usajili wa shule hayakuzingatiwa. Shule zimekua zikisajiliwa pasipokukidhi matakwa ya kiwango cha chini cha usajili, ambayo hujumuisha kuwepo kwa angalau vyumba 6 nya madarasa (kwa wanafunzi 40 kwa kila darasa) vyenye madawati ya kutosha pamoja na vyoo. Mfano wanafunzi takribani milioni 4 kati ya takribani milioni 8 hawakuwa na madarasa katika mwaka 2016; na wanafunzi takribani milioni 5 hawakuwa na vyoo. Aidha, madawati 243,000 kati ya 1,780,000 yalikosa madarasa ya kuwekwa na hivyo kuhifadhiwa nje.





- ii. Wahakiki wa Ubora wa Wizara ya Elimu walifanya ukaguzi ambao haukujumuisha uhakiki wa miundombinu katika shule za msingi. Hali hii imesababisha kuwepo kwa mazingira mabaya ya kujunzia kwa wanafunzi.
- iii. Kukosekana kwa kwa fedha za ukarabati kumechangia kuwepo kwa majengo chakavu katika shule za msingi na kushindwa kujenga miundombinu mipyä. Miongoni mwa sababu zinazochangia hali hii ni pamoja na kushuka kwa

bajeti ya sekta ya elimu kutoka 19% kwa mwaka 2012/13 hadi 17% kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka wa fedha wa 2013/14 hadi 2015/16.

- iv. Pamoja kuwepo kwa kanzidata ya rasilimali zilizopo na mahitaji Wizara ya Elimu na TAMISEMI hawana taarifa ya hali ya miundombinu hiyo. Vilevile, kunakosekana taarifa za shule zilizosajiliwa na zisizosajiliwa, shule zilizokaguliwa na ambazo hazikukaguliwa pamoja na orodha ya mahitaji ya msingi yakuzingatia wakati wa ukaguzi. Mfano, shule 3,473 hazikuwa katika rejestra ya shule za msingi ya wizara ya elimu.

Mapendekezo: *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iimirishe na kusimamia mifumo ya usajili wa shule za msingi na kaguzi zifanyike mara kwa mara ili kuhakikisha miundombinuni stahiki na bora inakuwepo. Aidha, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inatenge fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, na kuweka mfumo unaohakikisha rasilimali hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa.*

8.3 Usimamizi wa Samani za Barabara

Ukaguzi huu unahuusu usimamizi wa Samani za Barabara. Samani za Barabara ni neno linalowakilisha vibao, michoro na kingo za barabara. Hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko la matukio ya ajali za barabarani mathalani mwaka 2013 ziliripotiwa ajali takribani laki 7 ikilinganishwa na ajali milioni 1.2 zilizoripotiwa mwaka 2014 ikiwa ni ongezeko la ajali laki 5 sawa na asilimia 71 katika kipindi cha mwaka mmoja. Ajali za



barabarani zimekuwa ni moja ya chanzo cha vifo, majeruhi, ulemavu wa kudumu na uharibifu wa miundombinu.

8.3.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kuangalia ni kwa namna gani Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuititia Wakala wa barabara inasimamia kikamilifu uwekaji, utunzaji na matengenezo ya samani za barabara pamoja na uratibu baina ya watendaji na wadau wanaosimamia samani za barabarani.

8.3.2 Mapungufu yaliyobainika

- i. Asilimia 50 ya barabara zilizokaguliwa zenye jumla ya kilomita 1395 hazikuzingatia mahitaji ya kiusalama kwa watumiaji wa Barabara. Zoezi la ukaguzi lilihusisha barabara 8 za Tanzania bara ambazo ni barabara ya Igawa-Mbeya (km 330), Dodoma – Iringa (km 270), Morogoro – Dodoma (km 263), Chalinze – Tanga (km 248), Dar – Chalinze (km 99), Tanga – Horohoro (Km 72), Mbeya – Chunya (km 72) na Lindi – Mtwara (km 41).

Kati ya barabara hizi, barabara ya Tanga - Horohoro ilizingatia mahitaji ya kiusalama kwa watumiaji kuliko barabara zingine. Mfano; Barabara ya Dodoma- Iringa (eneo la Seluka na Mlowa shule za msingi) hapakua na alama ya kivuko cha waenda kwa miguu, Barabara ya Lindi-Mtwara (Mikindani) haikua na kingo ya barabara dhidi ya ukingo wa bahari, Mbeya- Iringa eneo la Igurusi kati ya Igawa na Mbeya ipo alama inayoonyesha kivuko

cha waenda kwa miguu lakini hapakua na Mchoro wa kivuko cha waenda kwa miguu. Aidha, barabara ya Morogoro - Dodoma, Dodoma - Iringa na barabara kuu ya TANZAM (Iringa - Mbeya) haina alama katika maeneo ya hatari kama vile mikunjo mikali, mwisho wa mwendo mkali na alama za uwezekano wa kuanguka kwa mawe.

- ii. Katika mwaka 2015/2016 mikoa saba kati ya nane haikuzingatia uwekaji wa samani za barabara kwa ajili ya watu wenyewe ulemavu licha ya Wakala wa Barabara kutenga fedha kiasi cha takribani shilingi milioni 310 kwa ajili ya kazi hiyo. Mkao wa Iringa pekee ndio uliofanikiwa kuweka samani za barabara kwa asilimia 100 katika barabara zote zilizo chini ya usimamizi wa TANROAD mkoa. TANROAD ilitoa kiasi cha shilingi milioni 33 kwa ajili ya kutekeleza jukumu hiyo katika barabara zote zilizo chini ya usimamizi wao. Barabara zilizofanikiwa ni pamoja na Iringa –dodoma, barabara kuu ya TANZAM (Igawa – Mbeya), Iringa –Mafinga hata hivyo mikoa mingine ilitumia fedha hizo kwa shughuli zingine. Mfano, mkao wa Mbeya ulipokea takribani shilingi milioni 45 kwa ajili ya alama 96 za walemovu lakini ni alama 12 tu ndio zilizowekwa. Aidha, Mtwara ilipokea takribani shilingi milioni 21 lakini haikuweka alama za walemovu kabisa.
- iii. Ni kaguzi 5 (8%) kati ya 66 za usalama barabarani zilizotakiwa kufanyika na Wizara pamoja TANROADS katika kipindi cha mwaka 2012 na 2016 ndizo zilifanyika. Hata hivyo, zaidi ya 75% ya mapendekezo ya kaguzi hizo zilizofanyika hayakutekelezwa hivyo fedha iliyotumika



haikutimiza malengo yaliyokusudiwa. Kutofanyika kwa kaguzi za usalama kumeathiri uwezo wa Wizara ya Ujenzi na TANROADS kutambua mahitaji ya kiusalama barabarani.

Mapendeleko: *TANROADS iimarishe usimamizi wa miradi ya barabara katika kila hatua na kushirikisha wadau muhimu wa usalama barabarani katika mipango ya uwekaji, utunzaji na matengenezo ya samani za barabara pamoja na kuweka mfumo wa ufuatilaji na mwongozo wa utoaji taarifa kwa ufanisi.*

8.4 Usimamizi wa Mikataba iliyoingiwa kati ya Serikali na Hospitali binafsi

Ukaguzi huu unahuusu usimamizi wa mikataba baina ya serikali na hospitali binafsi. Kati ya mwaka 2013/2014 hadi 2015/2016 takribani shilingi bilioni 276 zilipelekwa na serikali katika hospitali binafsi zenyе mkataba na serikali kama ruzuku ili kuziwezesha hospitali hizi kutoa huduma za afya kama zile za serikali katika ngazi husika.

Licha ya Serikali kutoa ruzuku kwa hospitali hizo kumekuwa na malalamiko toka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wananchi kuwa upatikania wa huduma katika hospitali hizi umekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa huduma zinazopatikana. Hospitali 8 zilizohusika katika ukaguzi huu ni zile Teule za halmashauri na Rufaa za kanda ambazo ni Nyangao (Halmashauri ya **Wilaya ya Lindi**),

Kolandoto (Halmashauri ya **Manispaa ya Shinyanga**), Sumve (Halmashauri ya **Wilaya ya Kwimba**), Kibosho (Halmashauri ya **Wilaya ya Moshi**) na Machame (Halmashauri ya **Wilaya ya Hai**). Aidha, hospitali za Rufaa za kanda zilijumuisha KCMC (Kanda ya Kaskazini), Bugando (Kanda ya Ziwa) na CCBRT (Kanda ya Mashariki).

SERIKALI INATOA
RUZUKU KWIA HOSPITALI
BINAFSI LAKINI HUDUMA
TUNAZOPATA MUNGU
NDO ANAJUA...



8.4.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kuangalia ikiwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais – TAMISEMI zimesimamia vyakutosha mikataba iliyoingiwa baina ya serikali na hospitali binafsi.



8.4.2 Mapungufu yaliyobanika

- i. Serikali haikuwa na mwongozo wa utayarishaji wa mikataba wala mkakati madhubuti kabla ya kusaini mikataba na hospitali binafsi. Haikufanya tathmini ya kuwepo kwa uhitaji wa hospitali ya hadhi hiyo katika halmashauri husika, jambo lililosababisha kuwepo kwa hospitali mbili zenye hadhi moja katika halmashauri moja.
- ii. Kutokuwepo uwazi kati ya Serikali na hospitali binafsi katika maandalizi ya mipango ya mwaka pamoja na bajeti. Kila upande unaandaa mipango yake bila kushirikisha upande mwingine kikamilifu. Hospitali hazonyeshi baadhi ya taarifa zake kwa Serikali kama vile Mapato yatokanayo na huduma wanayotoa.
- iii. Baadhi ya hospitali kutoa huduma zisizolingana na hadhi yake. Hii ilichangiwa na baadhi ya hospitali kukosa wahudumu wenye ujuzi na vifaa vinavyo hitajika katika huduma hizo. Aidha, hospitali haziweki wazi aina ya huduma wanazotoa pamoja na bei kwa kila huduma.
- iv. Bei elelezi za tangu mwaka 1997 zilizowekwa na serikali kwa huduma za zimepitwa na wakati. Hivyo kutozingatiwa na hospitali katika kupanga bei za huduma. Mfano katika hospitali teule za halmashauri bei elekezi kwa kipimo cha malaria kilikuwa ni shilingi 100, bei halisi kwa kipimo hicho kwa sasa ni wastani wa shilingi 2,000.

- v. Ufuatiliaji na tathmini ya mikataba ya hospitali haikufanywa ipasavyo na Wizara ya Afya na TAMISEMI. Mifumo ya ufuatiliaji ilikuwepo lakini haikutosheleza kwa sababu haikujumuisha masula ya mikataba ya hospitali. Mikataba iliyosainiwa haikufanyiwa tathmini na marejeo kwa wastani wa miaka 13 tangu isainiwe.

Mapendekezo: Wizara ya Afya na TAMISEMI zihakikishe zinasimamia ipasavyo mikataba waliyosini baina ya serikali na hospitali binafsi. Hii ni pamoja na kuhakikisha hospitali binafsi zilizosaini mikataba na serikali zinatoa huduma kulingana na hadhi sambamba na kuzingatia bei elekezi baada ya kurejewa.

8.5 Wahitimu wanaoanadaliwa kwenye Sekta ya Mafuta na Gesi Nchini

Ukaguzi huu unahu namna mifumo yetu ya elimu ya juu ilivyoweza kutafsiri mahitaji ya wataalam katika sekta ya Mafuta na Gesi Asilia katika mitaala yao ya elimu kwa lengo la kuaandaa wataalam wa kutosha na wenye ujuzi kwa ajili ya kusimamia sekta ya mafuta na gesi nchini.

8.5.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kutathmini kama Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina mfumo bora wa kuhakikisha idadi na ubora wa wahitimu wanaozalishwa inakidhi mahitaji ya sekta ya mafuta na gesi asilia; na kama taasisi za elimu nchini zina uwezo wa kuzalisha ujuzi unaohitajika katika sekta hiyo.



8.5.2 Mapungufu yaliyobainika

- i. Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia haina mipango na mikakati thabiti katika kuzalisha wataalamu katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Hii ni kwa sababu Wizara ya Elimu haikufanya uchambuzi wa kina kuchambua mahitaji ya ujuzi unaotakiwa katika mnyororo wa thamani wa mafuta na gesi asilia. Pia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Tume ya Vyuo Vikuu na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundii hawajafanya ufuatlia na tathimini ya kutosha ya shughuli za kutoa ujuzi katika sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo toka mwaka 2012 hadi 2016.
- ii. Uwezo mdogo wa taasisi zote sita zinazotoa elimu na mafunzo katika sekta ya mafuta na gesi nchini. Taasisi zote hazina uwezo wa kuzalisha wa wahitimu wenye ujuzi unaohitajika katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Asilimia 45 ya ujuzi wa kitaalamu unaohitajika katika mitaala ya vyuo vikuu vinavyotoa elimu katika sekta ya mafuta na gesi asili unakosekana. Mitaala inayotumika katika vyuo hivyo inakosa takribani ujuzi 10 zinazotakiwa katika ngazi ya vyuo vikuu. Kati ya taasisi 6 ni taasisi mbili (33%) zinatoa zinatoa kozi ya afya usalama mahala pa kazi na mazingira japokuwa kozi kuwa kozi hii ni muhimu kumuwezesha muhitimu kuajiriwa katika sekta ya mafuta na gesi.

- iii. Ukosefu wa miundombinu na vifaa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo. Vyuo vyote sita vilivyokaguliwa vinakabiliwa na upungufu wa vifaa na miundombinu (maabara, vifaa na zana) kwa ajili ya kutoa mafunzo. Kati ya vyuo sita vyuo 2 (33%) havikuwa na maabara kabisa wakati vyuo 3 (50%) vinakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya maabara.

Mapendekezo: *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iangalie upya mfumo wa usimamizi wa uzalishaji wa wataalamu wanaohitajika katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Hii ni pamoja na kuandaa mipango kwa ajili ya kusimamia shughuli zinazohusu kukuza ujuzi, kuaanda mfumo sahihi wa ufuatiliaji, uratibu na kuhakikisha kuna upatikanaji endelevu wa fedha za kutekeleza shughuli hizo. Aidha, Wizara ihakikishe tume ya vyuo vikuu na baraza la Taifa la ufundi inaandaa utaratibu wa kufuatilia na kuhakikisha mitaala ya taasisi za elimu na mafunzo inaanaliwa kwa ufanisi.*

8.6 Usimamizi wa Kagazi za Vyombo katika Usafiri wa Njia ya Maji

Ukagazi huu unahu su tathmini ya kagazi za vyombo vya usafiri kwa njia ya maji zinazofanywa na SUMATRA ili kubaini ni kwa kiasi kagazi hizo zimekusudiwa kupunguza tatizo la ajali za vyombo vya usafiri kwa njia ya maji.



8.6.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kutathmini ikiwa Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri kwa njia ya Maji na Nchi Kavu (SUMATRA) zinasimamia kikamilifu kaguzi za vyombo katika Usafiri wa njia ya maji Tanzania bara.

8.6.2 Mapungufu yaliyobainika

- i. Kukosekana kwa kanzidata ya usajili wa vyombo vidogo. SUMATRA haina kitabu cha usajili wa vyombo vidogo hii ilisababisha namba moja ya usajili kutolewa kwa zaidi ya vyombo viwili. Mfano namba TAN 001 ilipewa kwa vyombo LADY DIANA, 4 LADY DIANA na MV DELGO na namba TAN 008 ilitolewa kwa MV PEPI na MV ZABAR JADA. Pamoja na kuwepo kwa kitabu cha usajili wa vyombo vikubwa (meli) kuna vyombo vya usafiri ambavyo havitumiki na usajili wake haujafutwa.
- ii. SUMATRA ilifanya ukaguzi chini ya 20% ya vyombo vidogo vinavyofanya safari zake Tanzania Bara kwa mujibu wa sensa iliyoanyika mwaka 2012. Kipindi cha 2012/2013 vyombo vidogo ambavyo havikukaguliwa vilikuwa 80.06% wakati miaka iliyoftatia idadi ilipanda hadi kufikia 84.99%. Na mwaka 2015/2016 vyombo vidogo visivyokaguliwa viliongezeka hadi 87.86%.
- iii. SUMATRA haikutoa makatazo na adhabu kwa waendeshaji wa vyombo vya maji wasiozingatia viwango vya usalama kuanzia mwaka 2011/2012 hadi 2014/2015. Na mwaka 2015/2016 ni asilimia 1.85 tu ya wakosaji ndiyo walipewa adhabu.

iv. Kuanzia mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano haikufanya ufuutiliaji wa masuala ya usalama katika Usafiri wa njia ya maji mahsusini kwa kaguzi zinazosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Njia ya Maji na Nchi Kavu.

Mapendekezo: Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasilino iilagize SUMATRA, kusajili na kutoa leseni kwa vyombo vyote vidogo vyta usafiri wa maji, kuondoa katika kumbukumbu vyombo vyote visivytumika pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara.

8.7 Uendelezaji wa Maeneo ya Wazi yalioanisha Nchini

Ukaguzi huu unahu uudhibiti wa uendelezaji wa maeneo ya wazi yaliyoainishwa nchini kwa ajili ya matumizi ya umma. Ukaguzi uliangalia mamlaka za upangaji saba katoka katika kanda sita za kijiografia. Kanda ya Pwani, Kanda ya Ziwa, Mashariki, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kaskazini.

8.7.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kutambua maeneo ya wazi ambayo yalitengwa kwa ajili ya umma hayatumiki ipasavyo. Kutathhmini kama Ofisi ya Raisi-TAMISEMI kuitia mamlaka za upangaji wanatekeleza kwa ufanisi udhibiti wa uendelezaji wa maeneo ya wazi yalioanishwa nchini Maeneo ya wazi yalioanishwa katika mamlaka za upangaji kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya umma hayatumwi kwa mujibu wa mpango. Zaidi ya asilimia



80 ya maeneo ya wazi yaliyopangwa kwa ajili ya matumizi ya umma nchini yamevamiwa na hayaendelezwi.

8.7.2 Mapungufu yaliyobainika

- i. Mamlaka 6 (86%) za Mipango Miji kati ya 7 zilizotembelewa hazijaanza mchakato wa usajili wa maeneo ya wazi ya umma ili kutambua umiliki wake licha ya mamlaka hizo kuandikiwa na TAMISEMI barua ya tarehe 23 Oktoba, 2014 na kukumbushwa kwa barua ya tarehe 20 Januari 2015.
- ii. Maeneo ya wazi yaliyoanishwa kwa matumizi ya umma katika mamlaka za upangaji miji hayakulindwa na kudhibitiwa ili kuhakikisha yanatumika kama ilivyokusudiwa, badala yake maeneo yalibadilishwa matumizi; mfano kati ya maeneo 33 yaliyoainishwa na CDA kuwa maeneo ya wazi ya umma 17 kati ya hayo yaliidhinishiwa kwa matumizi ya bar. Vilevile, Mamlaka hazikuwa na mfumo wa kufuatilia na kuweka kumbukumbu za taarifa za wavamizi wa maeneo ya wazi ya umma.

Mapendekezo: Ofisi ya Rais - TAMISEMI iziagize mamlaka za mipango Miji kuimarisha udhibiti wa maeneo ya wazi ya umma ikiwa ni pamoja na kuyapatia hati miliki. Aidha, mamlaka hizi zinapaswa kushirikisha jamii kulinda maeneo ya wazi ya umma.

8.8 Usimamizi wa Usalama dhidi ya Moto katika Majengo ya Umma

Ukaguzi huu unahusu kuangalia kama Idara ya zima moto inasimamia matakwa ya usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma. Kumekua na matukio ya ajali za moto katika majengo ya umma, na kusababisha hasara kubwa zikiwemo upotevu maisha ya watu, majeruhi na kuharibika kwa mali. Ukaguzi ulihusisha vikosi 5 vya zima moto na uokoaji.

8.8.1 Lengo la ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kutathmini kama Jeshi la Zima Moto na Uokoaji limesimamia kikamilifu matakwa ya usalama dhidi ya moto katika majengo ya umma.

8.8.2 Mapungufu yaliyobainika

- i. Jengo la umma 1 kati ya 3 ambayo hakufanyiwa ukaguzi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walipewa cheti cha usalama dhidi ya moto kinyume na matakwa ya sharia. Aidha, Jeshi la Zimamoto halikua na mpango wa ukaguzi wa majengo ya umma dhidi ya matukio ya moto na hivyo kuwepo majengo yasiyokaguliwa kwa zaidi ya mwaka licha ya kuwepo kwa kanuni inayowataka kukagua makengo ya umma angalau mara moja kila mwaka.
- ii. Jeshi la Zimamoto halikufanya ukaguzi kwa ufanisi na hivyo kushindwa kubainisha mapungufu yaliyopo katika majengo yenye kuhatarisha usalama dhidi ya matukio ya moto. Kati ya majengo 20 yaliyokaguliwa na jeshi, majengo 11 yalikua na vifaa vya kuzima moto vilivyoisha



muda wa kutumika na kukosa vifaa vya kung'amua (kutambua) uwepo wa moshi. Majengo 7 Kati ya 11 hayakuwa na mabomba ya mipira kwa ajili ya kuzimia moto, kuzibwa kwa njia za dharura za kutokea wakati wa moto, ukosefu wa masuala haya huongeza na kufanya mazingira magumu kwa usalama dhidi ya moto. Hata hivyo, mapungufu haya hayakubainishwa katika taarifa za ukaguzi za jeshi la polisi. Pamoja na haya yote, jeshi la zima moto lilitoa hati ya salama kwa wamiliki wa majengo yasiyokidhi vigezo na matakwa ya usalama dhidi ya ajali za moto.

- iii. Jeshi la Zima Moto na Uokoaji iliwasilisha matokeo ya ukaguzi kwa wamiliki na au watumiaji wa majengo yenye mapungufu. Mapendekezo yaliyotolewa hayakuonesha viwango vya ubora, ukubwa na aina ya kifaa kinachotakiwa kuwekwa katika jengo husika. Hivyo hata kama mapendekezo ya ukaguzi yatafanyiwa kazi kuna uwezekano wa wamiliki au watumiaji wa majengo kuweka vifaa visivyo sahihi kwa ajili ya kujikinga dhidi ya moto.
- iv. Jeshi la Zima Moto na Uokoaji halikupitia michoro ya ujenzi na kutoa idhini wakati wa mchakato wa uidhinishaji wa michoro ya ujenzi unaofanywa na Halmashauri za Serikali za Mitaa. Pia Jeshi halikuchukua hatua za kuwakataza wananchi kujenga majengo pasipo idhini ya Jeshi hilo na kusababishwa majengo kujengwa pasipo kuzingatia matakwa ya usalama dhidi ya moto.

- v. Jeshi la zima moto na uokoaji halikufanya ufuatiliaji kwa wakati ili kutathmini hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wao. Mfano kati ya majengo 15 yaliyokaguliwa ufuatiliaji ulifanyika katika jengo 1 tu miezi miwili baada ya kupita kwa muda ulioainishwa jeshi hilo kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa mapendekezo yao. Vilevile, jeshi halikutoa adhabu kwa wamiliki wa majengo waliokiuka taratibu na matakwa ya usalama dhidi ya moto, hata hivyo, walifungua kesi dhidi ya wale waliochelewa kulipa au wasiolipa kabisa ada ya ukaguzi.

Mapendekezo: *Jeshi la zima moto na uokoaji lihakikishe linaimarisha usimamizi wa usalama dhidi ya moto ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Mamlaka za ramani za majengo katika kuhakisha ujenzi unazingatia matakwa dhidi ya moto.*

8.9 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi Ulifanyika na Kuwasilishwa bungeni Mwaka 2012 na 2013

Ukaguzi huu unahu matokeo ya ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye kaguzi 5 zilizopita na kuwasilishwa bungeni mwaka 2012 na 2013.

8.9.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi ni kufanya tathmini kubaini kiwango ambacho taasisi zilizokaguliwa zimetekeliza mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ukaguzi




huu wa kufuutilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na CAG kwa taasisi zilizofanywa Ukaguzi wa Ufanisi ni wa pili.

8.9.2 Mapungufu yaliyobainika

- i. Kati ya mapendekezo 107 yaliyotolewa na CAG kwa taasisi 8 katika kaguzi 5; mapendekeo 67 yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo 37 (35%) yalitekelezwa kwa kiasi na 30 (28%) hayakutekelezwa kabisa.
- ii. Upo udhaifu kwa Maafisa Masuuli kufuutilia na kutoa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za ufanisi zinazofanywa katika taasisi zao.

Mapendekezo: Ofisi ya Waziri Mkuu ihakikishe wizara, idara zinazojitegeme, wakala wa serikali na mamlaka za serikali za mitaa ihakikishe zinafanyiakazi mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi za ufanisi yanafuatiliwa na kutekelezwa vya kutosha na kwa ufanisi.

RIPOTI ZA KAGUZI MAALUM



KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2016

SURA YA TISA

9.0 RIPOTI ZA KAGUZI MAALUM

Sura hii inatoa taarifa ya Kaguzi Maalum zilizofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2016. Taarifa hii imejumuisha Kaguzi Maalum za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

9.1 **Ukaguzi wa Serikali Kuu**

Kaguzi Maalum mbili zilifanyika ni Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Fedha za GAVI Alliance kwa ajili ya chanjo ya Surua Rubella.

9.1.1 **Matokeo ya Ukaguzi wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA)**

- i. Fomu 7,762,907 zilizochapishwa na mpiga chapa binafsi kwa takribani shilingi bilioni 2 zilizopokelewa na Mamlaka (NIDA) na hazikutumika.
- ii. Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya takribani shilingi milioni 63 ulifanyika kwa kutumia ushindanishi wa wazabuni wa kughushi. Mchakato wa kumpata mshauri elekezi wa mradi na uingiwaji wa mkataba wake haukuwa sahihi. Aidha, ilibainika kuwa uongozi, wafanyakazi na wazabuni walishiriki kwa namna moja au nyiningine katika ubadhirifu na udanganyifu kwenye matumizi ya fedha katika mradi wa kuboredha Vitambulisho vya Taifa.

Mapendekezo: Ofisi ya Waziri Mkuu iimarishe Idara ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali ili nyaraka zote za serikali ziweze kuchapwishwa katika ofisi hiyo. Pia, hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watumishi waliohusika katika udanganyifu huo sanjari na kuhakikisha watumishi hao wanafidia hasara iliyopatikana.

9.1.2 Matokeo ya ukaguzi wa chanjo ya Surua Rubella

Miongoni mwa matatizo yaliyobainika katika ukaguzi huu ni pamoja na matumizi ya takribani shilingi bilioni 1 ya fedha zilizotolewa na Gavi Alliance kwa Wizara ya Afya kwa ajili ya Chanjo ya Surua Rubella hazikuthibitika kupokelewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 1 zilitumika kulipa posho hewa kwa kutumia nyaraka za kughushi, shilingi milioni 294 zililipwa kwa watumishi hewa ambao hawakuhusika katika zoezi la chanjo na shilingi milioni 316 zililipwa kwa ajili ya huduma hewa ya chakula. Hii inaashiria udanganyifu na vitendo vya rushwa katika usimamizi wa utekelezaji wa mradi wa Chanjo.

Mapendekezo: Hatua za kinidhamu na za kisheria zichukuliwe na mamklaka husika dhidi ya wahusika. Vilevile, fedha zilizolipwa kwa nyaraka za kughushi zirejeshwe na wahusika waliotenda kosa hilo. Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai ifuatilie kwa karibu uhalali wa matumizi ya fedha ambazo zilionekana kulipwa kwa maafisa wa mamlaka za serikali za mitaa ambao walikanusha kuyafahamu malipo hayo.



9.2 Mashirika ya Umma

Sehemu hii inahusu taarifa za kaguzi maalum za Mashirika ya Umma.

9.2.1 Taarifa za Ugazzi Maalumu Kuhusu Sekta ya Mafuta na Gesi

Ilibainika kuwa bomba la gesi asilia linatumika kwa 6% tu ya uwezo wake wa kusafirisha gesi. Hali hii imesababishwa na kutozingatiwa kwa mkataba kati ya TPDC na TANESCO ulioitaka TANESCO kuhamkisha kwamba uzalishaji wa umeme kwa mitambo yake sita (Kinyerezi I, Kinyerezi II, Ubungo I, Ubungo II, Tegeta na Symbion) inatumia gesi asilia kuzalisha umeme. Ilibainika kuwa ni mtambo wa Kinyerezi I unaotumia gesi asilia ya bomba hili kuzalisha umeme.

Mapendekezo: *Wizara ya Nishati, Madini TPDC na TANESCO wahakikisha kwamba kiwango cha matumizi ya gesi inayosafirishwa kwenye bomba la gesi asilia kinafikia asilimia iliyokusudiwia kwenye mikataba. Kinyerezi I*

9.2.2 Mkataba katika TPDC na PAET

- i. Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (TPDC) limeingia mkataba na kampuni ya Pan African Energy Tanzania Limited (PAET) usio na tija kwa Umma. Mkataba huu ni Mkataba wa Ubia wa Uzalishaji wa Gesi (PSA) baina ya TPDC na PAET ambapo kadiri uzalishaji wa gesi asilia unavyoongezeka ndivyo gawiyo la serikali linazidi

kupungua.

- ii. Kampuni ya PAET hailipi mrahaba kwa serikali badala yake TPDC ndiyo hulipa mrahaba huo. Hii hutokana na makubaliano kuwa PAET inakata kodi zote kutoka katika mapato yake kama gharama za uendeshaji na uwekezaji na hivyo kuifanya PAET kutolipa kodi yoyote kwa serikali katika kipindi chote cha mkataba.
- iii. Mikataba 18 ya uchimbaji gesi (PSA) imewapa haki wawekezaji kuendelea kumiliki mali zinazohamishika baada ya kumaliza mkataba licha ya kuwa gharama hizo zimekwisha rejeshwa. Suala hili pia lipo katika mikataba ya madini.

Mapendekezo: Serikali ipitie upya mkataba na kufanyika makubaliano mapya ya mgawanyo wa uzalishaji (PSA) ili kuiwezesha Serikali kunufaika pindi uzalishaji unapoongezeka na PAET kulipa mrahaba na kodi. Aidha, Serikali ihakikishe inamiliki mali zinazohamishika na zisizohamishika baada ya kipindi cha mkataba kwa kuwa gharamazake zimesharejeshwa na Serikali.



9.2.3 Mamlaka ya Bandari Tanzania



Mamlaka ya Bandari ilipoteza takribani shilingi bilioni 6 kwa kutokusanya mapato yatokanayo na ushuru wa bandari. Hii ilisababishwa na ubadhirifu uliohusisha makampuni ya kutoa mizigo bandarini, wafanyakazi wa Mamlaka na watumishi wa taasisi za benki.

Mapendeleko: *Mamlaka ya Bandari kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na mabenki husika kuhakikisha kwamba fedha hizi zinarejeshwa.*

MAWASILIANO

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, 16 Barabara ya Samora,

S.L.P. 9080,11101 Dar es Salaam.

Simu ya Upepo: ‘Ukaguzi’ D’Salaam,

Simu: 255 (022) 2115157/8,

Tarakishi: 255 (022) 2117527,

Barua pepe: *mwananchi@nao.go.tz* au *info@nao.go.tz*,

Tovuti: *www.nao.go.tz*